SportPesa
CHEZA USHINDE SASA
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



UKURASA 3

**WAZEE** watoa kilio kwa kutelekezewa wajukuu




Nipashe
Jumatatu Januari 24, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580835
MWANGA WA JAMII
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

UKURASA 11

# MAUAJI YA KUTISHA

**WANAFAMILIA** watano wauawa na wasiojulikana, miili yakutwa ndani ya nyumba...*Endelea ukurasa 2*



UKURASA WA 3

## KIFUSI CHAUA, KUJERUHI WATOTO

KIFUSI kimeua mtoto mmoja na kumjeruhi mwenzake walipokuwa wakichimba...

UKURASA WA 7

## WALIOSHTAKIWA KULIMA BANGI WAACHIWA HURU

MAHAKAMA Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi, imewaachia huru washtakiwa wawili waliokuwa...

UKURASA WA 8

## WANAOJIFUNGULIA NYUMBANI KUTOZWA FAINI 50,000/-

VIJIJI sita katika kata ya Ubagwe Halmashauri ya Ushetu mkoani Shinyanga, vimeweka utaratibu wa kumtoza faini ya Sh. 50,000 mjamzito atakayebainika...




Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi (kulia) na Jaji Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahim Hamis Juma, wakiondoa pazia kuashiria uzinduzi wa nembo ya Mahakama Kuu na Wiki ya Sheria Tanzania, hafla iliyofanyika viwanja vya Nyerere Square jijini Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

UKURASA 2

# Rais Mwinyi ahimiza mabadiliko ya sheria




Katibu Mkuu wa Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale Zanzibar, Fatma Mbarouk Khamis (wapili kulia), akibadilishana mkataba wa makubaliano ya ushirikiano wa wizara hiyo na Ofisa Mkuu wa Biashara na Wateja Binafsi NMB, Filibert Mponzi, wakati wa kusainiana mkataba huo mjini Zanzibar. Wapili kushoto ni Meneja wa Tawi la NMB na Kaimu Meneja wa Biashara Zanzibar, Naima Shaame, (kushoto) ni Mkuu wa Biashara ya Kadi NMB Zanzibar, Philbert Cashir na (kulia) ni Katibu Mtendaji wa Kamisheni ya Utalii Zanzibar, Hafsa Mbamba. **Habari Uk. 7**

## RIPOTI MAALUM

## Kina Ziwa Tanganyika kilivyoliza wajasiriamali

UKURASA 4

**MICHEZO** SIMBA YAKIRI UBUTU KWA MASTRAIKA WAKE UK.23 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Rais Mwinyi ahimiza mabadiliko ya sheria

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amefungua milango kwa wanasheria nchini kuitumia wiki ya sheria kuzishauri serikali kuhusu sheria kinzani ili zifanyiwe marekebisho na kuleta tija kwa jamii.

Aidha, amewataka watumishi wa Mahakama kuwa mstari wa mbele kupiga vita rushwa na kuwajibika ipasavyo ili kutoa haki ya utumishi kwa wananchi.

Rais Dk. Mwinyi aliyasema hayo jana wakati akizindua maadhimisho ya Wiki ya Sheria katika viwanja vya Nyerere Square jijini Dodoma.

Alisema ana uhakika wanasheria wanajua sheria ambazo ni kinzani, hivyo watumie wiki hii kuishauri serikali ya Tanzania Bara na Zanzibar kuhusu sheria hizo nao kama viongozi watazifanyia kazi ipasavyo ili ziweze kuleta matumaini kwa wananchi.

Alisema kuna changamoto ambazo ni kikwazo katika sheria kwa hiyo wao kama wanasheria waishauri serikali kupitia mijadala na wao watayafanyia kazi kwa maslahi ya taifa.

"Nawashauri wanasheria kutumia hii wiki kuangalia sheria kinzani, tunahitaji kuona sheria zinakuwa katika mstari ili ziwe na tija kwa wananchi,"alisema Dk. Mwinyi.

Kadhalika, Dk. Mwinyi akizungumzia kuhusu vitendo vya rushwa akisema watumishi wawajibike kikamilifu ili kukuza uchumi wa nchi hususani uchumi wa bluu.

Alisema rushwa ni adui wa haki na inarudisha maendeleo nyuma, hivyo watumishi wanapaswa kufuata sheria katika uwajibikaji wao ili kuleta maendeleo katika taifa.

"Nawaomba mpige vita rushwa kwa sababu ni adui wa haki na inarudisha nyuma maendeleo ya nchi," alisema Dk. Mwinyi.

Alisema mafanikio ya kiuchumi, kibiashara hutegemea kuwapo na misingi ya utawala wa sheria ya uhuru wa Mahakama.

Pia alisema kwa upande wa serikali ya Mapinduzi Zanzibar dhamira ni kujenga uchumi wa kisasa unaozingatia raslimali za dhahabu na uchumi wa bluu, na kwamba serikali yake itawasaidia kujenga uchumi wa kisasa.

Alisema serikali zote mbili zinategemea uwezeshi na michango mikubwa ya sekta ya sheria na hasa kufuata ushauri wa kitaalamu kutoka kwa wanasheria.

Aliwata wanasheria watumie fursa kutoa wito kwa jamii kuielewa sheria na kuifanyia kazi ikiwamo mipango ya uchumi na kutoa ushauri wa kisheria serikalini.

"Novemba 11, 2021, katika hotuba yangu niliweka wazi dhamira ya kuijenga Zanzibar yenye uchumi wa bluu na uchumi huo ni matumizi endelevu ya rasilimali za bahari, ambapo huo ni uchumi unaofungamanisha kwa pamoja sekta za uvuvi, ukulima, uchimbaji wa mafuta na gesi pamoja na utalii wa fukwe,"alisema.

Alisema Zanzibar inahaja ya kufanya mabadiliko ya kiuchumi kwa kuzitumia ipasavyo rasilimali za bahari kutokana na kuwapo kwa udogo wa ardhi, huku idadi ya watu ikiendelea kuongezeka.

**MASHAURI MAHAKAMANI**

Aliwataka watumishi wa Mahakama kuongeza kasi ya usikilizaji wa mashauri hayo ili kupunguza msongamano katika mahakama mbalimbali.

Aliwapongeza kwa kuanzisha mahakama inayotembea, kwani imesaidia sana kuwafikia wananchi wa maeneo mbalimbali na kupongeza kwa hatua zilizochukuliwa kutafsiri sheria kwa lugha ya

Kiswahili, jambo ambalo linawapa matumaini Watanzania.

"Ni vema sasa kuongeza jitihada za kupata wataalamu wa lugha ya alama pamoja na kuimarisha miundombinu inayozingatia uwapo wa Watanzania wenye uhitaji maalumu.

"Binafsi nimeridhishwa sana na ushirikiano wa mahakama ya Bara na Visiwani tokea 1965 unaendelezwa kwa kupeana uzoefu na utaalamu na ninatoa wito wa kuendeleza uhusiano huo na kuongeza kasi ya ufanisi katika mahakama hizo,"alisema Dk. Mwinyi.

Hata hivyo, aliwasihi watumishi wa Mahakama pamoja na jamii kwa ujumla kuhakikisha wanakwenda kupata chanjo ya UVIKO-19 ambayo ni muhimu kwa afya ya jamii.

Jaji Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahim Juma, alisema wana mpango wa kubadili mbinu za utoaji huduma za kimahama na kisheria ili wasiachwe nyuma ya mapinduzi ya nne ya viwanda.

Aliwataka wanasheria kujifunza na kuufahamu uchumi wa bluu unaojengwa Zanzibar kwa kuwa wakizielewa sera na mipango watakuwa na nafasi nzuri ya kushauri na kushughulikia aina mpya ya mashauri ambayo yanaweza kuibuka na kuhitaji ujuzi na maarifa, tofauti na ilivyozoeleka.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akishika maji wakati alipoweka jiwe la msingi la mradi wa maji wa Mogitu-Katesh wilayani Hanang' katika ziara ya Mkoa wa Manyara jana. Kushoto ni Waziri wa Maji, Juma Aweso. **PICHA: OFISI YA WAZIRI MKUU**

# MAUAJI YA KUTISHA

**Paul Mabeja na Renatha Msungu ,** DODOMA

WATU watano wa familia moja wakazi wa Kijiji cha Zanka, wilayani Bahi, wameuawa kikatili na watu wasiojulikana huku miili yao ikikutwa ndani ya nyumba yao ikiwa imeanza kuharibika.

Miili ya watu hao imetambuliwa kuwa ni ya Hoseah Kapande, baba wa familia hiyo na mkewe Paulina Kapande.

Wengine ni watoto wawili na mjukuu ambao ni Isack Kapande, mwanafunzi wa kidato cha kwanza, Agnes Kapande, mwanafunzi wa darasa la tatu na mjukuu aliyejulikana kwa jina moja la Heltony, mwanafunzi wa darasa la nne.

Akizungumza katika eneo la tukio juzi, mdogo wa marehemu Ernest Kapande, alisema mara ya mwisho kumuona kaka yake na familia ilikuwa Januari 20, mwaka huu.

Alisema hawajaonana tena hadi juzi alipopata taarifa kuwa kaka yake pamoja na familia yake wamekutwa wameuawa ndani ya nyumba yao. "Mimi marehemu ni kaka yangu, mara ya mwisho kumuona ilikuwa ni juzi, lakini baada ya hapo hatukuonana tena," alisema.

Alisema taarifa za kifo cha kaka yake amezipata kutoka kwa mtoto wake baada ya kumpigia simu kumweleza kuwa baba yake mkubwa amekutwa amekufa ndani ya nyumba na familia yake.

Mwenyekiti wa serikali ya kijiji hicho, Yohana Japheti, alisema, taarifa za tukio hilo wamezipata juzi majira ya saa 10 jioni baada ya watoto wa shule kutoa taarifa.

"Watoto wadogo wa shule ndiyo walianza kupiga kelele baada ya kuona miili ya marehemu ikiwa ndani na kuanza kutoa harufu ndipo na sisi tukazitoa taarifa kwa mkuu wa kituo cha polisi," alisema mwenyekiti huyo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Onesmo Lyanga, akizungumza na waandishi wa habari katika eneo la tukio juzi, alithibitisha tukio hilo na kusema taarifa za awali zinaonyesha watu hao wameuawa na watu wasiojulikana.

Kamanda Lyanga, alisema kutokana na mauaji hayo Jeshi la Polisi linaendelea na uchunguzi huku ikiwataka wananchi wa eneo hilo kuwa watulivu.

Vile vile, aliwataka wananchi wa eneo hilo kuwa mstari wa mbele katika utoaji taarifa wa matukio mbalimbali ya kihalifu yanayofanywa ndani ya jamii.

"Kumekuwa na matukio mengi ya mauaji ya kificho, jeshi limejipanga kuwasaka wahalifu wa matukio hayo," alisema Kamanda Lyanga.

Alisema Jeshi la Polisi liko imara kuhakikisha linawakamata wahalifu wote wanaofanya matukio hayo ya kikatili.

Alisema lengo lao ni kuona wananchi wa maeneo ya mijini na vijijini wanaishi bila wasiwasi na kwamba ni vyema watoe ushirikiano ili Dodoma iwe salama.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Antony Mtaka, aliviagiza vyombo vya ulinzi na usalama kufanya uchunguzi wa matukio hayo ambayo yanakatisha maisha ya watu.

Pia aliwataka ndugu kutoa ushirikiano wa kuwasaka wahalifu waliofanya tukio hilo lililosababisha familia hiyo kupoteza maisha.

Alisema wanahitaji kuona Dodoma inakuwa salama na kuongeza kuwa vyombo vya ulinzi na usalama viendelee kupambana na wahalifu hao ambao wanaikatili jamii.

Mmoja wa wakazi wa eneo hilo, Neema Mbuva, alisema mauaji hayo yemechangia kwa kiasi kikubwa kukatisha ndoto za wanafamilia hao.

Alisema wanakijiji wa eneo hilo wamesikitishwa na mauaji hayo na kuliomba Jeshi la Polisi kufanya uchunguzi ili kuwabaini wahalifu hao.

Alisema maeneo ya pembezoni mwa mji kumekuwa na mauaji ya kikatili kutokana na kila wanapofanya vitendo hivyo wanajificha na kushindwa kukamatwa.

Kadhalika, aliliomba jeshi hilo kuwasaidia wananchi ili wahalifu hao wakamatwe na kupewa adhabu kali liwe fundisho kwa wengine wanaofanya vitendo hivyo.

Hili ni tukio la tatu la mauaji mkoani Dodoma, matukio mengine yaliyotokea hivi karibuni ni wanawake wawili kuuawa na wapenzi wao kutokana na ugomvi wa kifamilia.

## HABARI KITAIFA

# Wazee walia kutelekezewa wajukuu

**Na Elizabeth Zaya,** HANDENI

BAADHI ya wazee walio kwenye Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini unaosimamiwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), wilayani Handeni, mkoani Tanga, wamesimulia mpango huo ulivyowasaidia kulea wajukuu wao waliotelekezwa na watoto wao.

Wakizungumza mbele ya maofisa wa TASAF waliowatembelea wazee hao, walisema baada ya kutelekezewa wajukuu waliishi maisha magumu ya kuwalea, lakini kwa msaada wa mpango huo, imekuwa rahisi kuwalea na kuwahudumia kwa mahitaji yote ya msingi.

Elizabeth Mganga (70), mkazi wa mtaa wa Kampene, Kata ya Kidereko, alisema aliachiwa mjukuu tangu akisoma chekechea, wakati mwingine alilazimika kuomba chakula kwa majirani kwa kuwa hakuwa na uwezo.

"Mtoto wangu alikuwa ameolewa, lakini bahati mbaya akafariki na alikuwa na mtoto mmoja, baada ya hapo familia wakakubaliana kwamba mtoto ataishi na baba yake mzazi kwa sababu mimi sina nguvu za kumtunza, lakini cha kushangaza baba yake alikuja akamtelekeza hapa kwangu na kuondoka zake," alisema Mganga.

"Nilijua labda atakuwa analeta hata pesa au chakula kwa ajili ya mtoto, lakini haikuwa hivyo, kwa hiyo nikawa nahangaika, hata mlo mmoja kwetu ilikuwa ni shida, mara nyingi tulikuwa tunakunywa uji na njaa ikizidi inabidi niende tu kwa majirani niwaombe wanisaidie na ukikuta msamaria mwema anakupatia hata pesa ukanunue chakula hata cha siku mbili, shuleni mtoto wakati mwingine alikuwa haendi kwa sababu ya njaa."

Kwa mujibu wa Mganga, tangu alipoingizwa kwenye mpango wa kunusuru kaya maskini, maisha yake yamekuwa bora kwa kuwa anapata milo mitatu kwa siku, na kumtunza mjukuu wake ambaye kwa sasa anasoma kidato cha sita na amejenga nyumba ya vyumba viwili baada ya kutunza pesa kidogo kidogo.

"Naishukuru sana TASAF, bila hivyo sijui maisha yangu yangekuwaje, hata hii afya niliyonayo ni kwa sababu mpango huu umeniwezesha nakula vizuri na nalala pazuri," alibainisha Mganga.

Amina Mwaliko (64), mkazi wa Msasa Shule, Handeni, alisema alitelekezewa wajukuu sita na kujikuta akiishi maisha magumu kutokana na kipato chake kuwa kidogo. "Maisha yangu nilikuwa nayaendesha kwa kutegemea kuuza mboga za majani mitaani na kipindi kile nilikuwa naishi maisha yangu ya kawaida kwa sababu sikuwa na familia kubwa, lakini hali ilianza kuwa ngumu baada ya kutelekezewa wajukuu sita ambao ni wa watoto wangu wawili, hawakuwa wanawajali kwa chochote na hivyo hali ikawa ngumu hata chakula kikawa cha taabu," alisema Mwaliko.

"TASAF ndiyo ilikuja kunikomboa kupitia mkutano wa kijiji ambao ulinipendekeza baada ya kuona hali ya maisha niliyokuwa nayo. Huu mpango niliuona kama mkombozi wangu, umenisaidia sana, kwa sasa maisha yangu ni mazuri na kupitia pesa kidogo ninayopewa nimejibana na kuanzisha biashara ndogo na nafuga kuku, tunaishi vizuri," alisema Mwaliko.

## Kifusi chaua, kujeruhi watoto wakitafuta mahitaji ya shuleni

**Na Lilian Lugakingira,** MULEBA

KIFUSI kimeua mtoto mmoja na kumjeruhi mwenzake walipokuwa wakichimba mchanga kujipatia mahitaji ya kuanza kidato cha kwanza.

Justine Abson (14) amekufa, huku mwenzake Carlos Shubi (14), akijeruhiwa sehemu mbalimbali za mwili wake ikiwamo miguuni na mgongoni, baada ya kuangukiwa na kifusi hicho.

Watoto hao walikuwa wakichimba mchanga katika Kijiji cha Buhaya Kata ya Kagoma, Wilaya ya Muleba, mkoani Kagera.

Akizungumzia tukio hilo, Mkuu wa Wilaya ya Muleba, Toba Nguvila, alisema lilitokea Januari Ijumaa saa 3:30 asubuhi, wakati watoto hao wakichimba mchanga kwa ajili ya kuuza ili wapate fedha za kununulia mahitaji madogo ya shule.

"Watoto hawa walikuwa wamechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika Shule ya Sekondari Buhaya, ni shule mpya imejengwa kwa fedha za UVIKO-19, na imeelezwa kwamba walikuwa wanatafuta pesa kwa ajili ya kununulia mahitaji madogo ya shule ikiwamo madaftari na viatu, ili Jumatatu (leo) waende kuanza masomo," alisema Nguvila.

Alisema taarifa za watoto hao kufukiwa na kifusi cha mchanga zilitolewa na wananchi, na kwamba walipotolewa kwenye kifusi hicho Justine alikuwa ameshapoteza maisha, lakini Carlos alikuwa hai, hivyo kukimbizwa Hospitali ya Kagondo ambako anaendelea na matibabu.

### KUMBUKUMBU YA KIFO



216664002

**PALME MAKOYE, 23/01/2022** umetimiza miaka 15 tangu ututoke duniani.Tarehe hii haitasahaulika kamwe maishani mwetu.Bado upo katika nafsi zetu na mawazo yetu.Sala na maombi yetu yapo kwako.Upendo,ukarimu na heshima ulizokuwa nazo vinatufanya uendelee kukumbukwa na kila mtu uliyekuwa karibu naye.

Unakumbukwa daima na wazazi wako,dada na kaka zako,ukoo wote wa Mwiza na Itule,ndugu jamaa na marafiki pamoja na majirani zako.

**"RAHA YA MILELE UMPE EE BWANA NA MWANGA WA MILELE UMWANGAZIE,APUMZIKE KWA AMANI".**

**TANGAZO LA MKUTANO WA MWISHO WA WANAHISA WA KAMPUNI YA**

**SAUTI YA UZIMA RADIO COMPANY LIMITED**

**CHETI CHA USAJILI NO.125531**

**Sheria ya makampuni, 2002 [kifungu 334[1]]**

Umma na wahusika wanafahamishwa kutakua na mkutano mkuu wa mwisho wa wanahisa wa kampuni **SAUTI YA UZIMA RADIO COMPANY LIMITED,** yenye usajili namba 125531 kitakachofanyika tarehe 09/02/2022 ofisini kwa mfilisi saa 4:30 asubuhi ambapo mfilisi atatoa hesabu ya kufungwa kwa hiari kwa kampuni.

| | |
|---|---|
| Mfilisi : | LINDA ALLAN MWAMBETE |
| Anwani ya mfilisi: | 368 MSASANI ROAD<br>MIKUMI HOUSE<br>OYSTERBAY<br>P.O. BOX 9673<br>DAR ES SALAAM<br>TANZANIA |
| Tarehe ya kuchaguliwa: | 09 APRIL 2021 |
| Amechaguliwa na : | WAMILIKI WA KAMPUNI |

Sahihi...................................

Tarehe......................................

**Jina: LINDA ALLAN MWAMBETE**

**Imetolewa na;**
**LINDA ALLAN MWAMBETE**
**SAUTI YA UZIMA RADIO COMPANY LIMITED**

216662502

**TANGAZO!!**
**AFRIWELD INDUSTRIES LTD**
**Nafasi ya kazi**

Wanahitajika wasichana Wenye umri kuanzia miaka 25-35

**Nafasi:** Mauzo

MSHAHARA wa kuvutia utatolewa!! wahi sasa Kupata nafasi nzuri!!

Kwa mwasiliano zaidi piga simu namba: **0719 184 070**

Piga simu muda wa kazi TU saa MBILI mpaka saa KUMI NA MOJA jioni

01/01/2022 MPAKA 31/01/2022

**Asante**

116653602

A PRODUCT OF The Coca-Cola Company

KILIMANJARO DRINKING WATER

**TAARIFA KWA UMMA**

**BONITE BOTTLERS LTD** inapenda kuufahamisha umma juu ya kusitisha matumizi ya **plastiki laini (seal)** katika vifuniko vya chupa za **Maji ya Kilimanjaro** kutokana na agizo la serikali juu ya matumizi ya plastiki hizi kulinda mazingira.




@kilimanjaro_drinking_water | kilimanjarodrinkingwater | kdw@bbl.co.tz

+255 762628166 | +255 659785276 | +255 272754422

RIPOTI MAALUM

# Mabadiliko tabianchi yalivyoathiri Ziwa Tanganyika

## ■Kina chaongezeka, wanawake wajasiriamali wakwama biashara ya samaki, washindwa kupeleka watoto shule...

Na Salome Kitomari, KIGOMA

MAISHA yetu yamebadilika sana kiuchumi, kwa sasa kupata Sh. 2,000 kwa siku ni ngumu sana, hatuna shughuli za kufanya kama zamani, kuongezeka kwa kina cha maji ya Ziwa Tanganyika kumeacha maumivu kwenye maisha yetu, hadi sasa baadhi yetu watoto wameshindwa kwenda shuleni kwa sababu tumeshindwa kuwanunulia sare na mahitaji mengine," ndivyo wanavyoeleza baadhi ya wanawake wajasiriamali eneo la Mwalo wa Kibirizi, mkaoni Kigoma.

Wanawake hao ambao wamelazimika kubadili biashara na kuuza maandazi na kufuma mashuka, wanasema ni kawaida kula mlo mmoja kwa siku wa saa 10 jioni, kutokana na hali ngumu huku mtaji ukiisha kwa kuwa ndiyo unaotumika kutunza familia siku wanayokosa fedha.

Miongoni mwao wapo waliofanya biashara hiyo kwa zaidi ya miaka 29, lakini mabadilikio ya tabianchi yamewalazimu kujifunza shughuli mbadala za kuwaingizia kipato huku wengine wakiwa tegemezi wa ndugu zao.

Mialo ya Kibirizi na Nyobonzi ni maeneo rasmi yaliyo na miundombinu muhimu ya kuwawezesha wakulima kuchakata, kubanika samaki, majiko maalum ya kukausha dagaa na kupika samaki, kuna sehemu ya kupokelea, kukaushia na nyavu za juu za kuanika ambao unaruhusu kukauka bila kuingia mchanga pia inaruhusu upepo kupita chini na juu.

Mkoa wa Kigoma uchumi wake unategemea uvuvi na kilimo, na kwamba mabadiliko ya tabianchi yamesababishia kiwango cha dagaa na samaki wa kutosheleza wananchi na biashara kuwa ndogo, kiasi cha kushindwa kupata mapato.

Mlasi Juma kwa jina maarufu Mrisho anayefanyabiashara ya samaki wabichi kwa muda mrefu eneo la Forodha ya Ujiji, anasema wameathirika kisaikolojia kwa muda mfupi kutokana na maji kufunika maeneo yao yote muhimu kwa biashara.

"Tumevamiwa na maji kutoka mahala pake kwenda kwingine, tulikuwa tunafanyabiashara kwenye jumba maalum, tulikuwa tunauza sana, lakini baada ya maji kutuvamia tuliachana na jengo lile na kuhamia upande wa pili, ambako sio eneo la biashara," anasema.

Aidha, anasema kutokana na hali hiyo mwalo wa Kibirizi umeathirika kwa kiasi kikubwa kwa kuwa nyumba ziliingiliwa na maji na kulazimu baadhi ya watu kutawanyika.

"Sehemu ya kuuzia mboga ilibadilishwa na kwenda kwingine watu wako mitaa ya Mitimingi, Kabondo, Pilimahonda na wengine tumebaki Forodhani, ingawa ni kugumu kupata biashara, lakini tuna afadhali kubwa ukilinganisha na wengine," anasema Mlasi.



Mwonekano wa Chuo cha Uvuvi Kigoma (FETA), Kibilizi, Kigoma Ujiji kilichozingirwa na maji, wanaonekana kwenye ngalawa ni wavuvi wakijiandaa kwenda kuvua. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

"Maji yamekuwa mengi hadi yametengeneza bwawa, zamani unanunua samaki za 40,000 una uhakika wa kuuza na kupata faida ya Sh. 5,000 au zaidi kwa siku, lakini kwa sasa sipati fedha yoyote kwa kuwa eneo letu limemezwa na maji na wavuvi hawapati samaki, zamani ukiwa Kando ya Ziwa ukiona mtumbwi unampungia mkono anasimama anakuuzia samaki kwa sababu tulikuwa kando ya ziwa, lakini sasa tuko mbali huku sokoni hauwezi kupata," anasema.

"Hali yangu kiuchumi imekuwa ngumu sana, sasa sina uhakika wa kipato, tupo mbali ambako mtumbwi hauwezi kufika, pia wavuvi wanapata samaki wachache sana, nasi tunakosa wa kuuza wanaenda kuuza kwingine," anasema.

Anasema kabla ya maji kujaa mwaloni alinunua samaki wa Sh. 60,000 ambao akiuza wote anapata faida ya Sh. 10,000 ya kwenda kula na familia yake.

**WAHANGAIKA KUPATA SH. 2,000**

"Kwa sasa unaweza kuwa na samaki wa Sh. 10,000, lakini kupata Sh. 2,000 ni kazi, familia zinahangaika kiasi cha kula mlo mmoja ambao huliwa saa 10 jioni kwa siku na unamshukuru Mungu kwa kuwa fedha inayopatikana ni ndogo kutosheleza mahitaji ya familia," anabainisha.

"Wewe ndiyo mama, familia inakuangalia wewe kwa kila kitu. Tunapigana sana kimaisha usiku na mchana tunamwomba Mungu atusaidie mwalo wetu wa Kibirizi urudi kama zamani kama tunavyoahidiwa kuwa bandari ipo na itarudi, tunamuomba Mungu irudi," anasema mjasiriamali huyo.

Kwa mujibu wa Mlasi, wazee wa zamani walisema maji yalikuwa eneo hilo na jingine kiasi cha wengi kushangaa maji yamerudi, eneo kubwa lilikuwa na makazi ya watu wanapanda boti kwenda, lakini yote yamemezwa na maji kidogo kidogo na sasa watu hawaishi tena.

Aidha, anasema alianza biashara hiyo mwaka 2000 na akilinganisha biashara ya wakati huo na sasa hali ya maisha ni ngumu. "Nilikuwa ninkinunua mzigo wa Sh. 100,000 nikiingia nao sokoni nina uhakika wa kuumaliza na kupata riziki ya kula na watoto unapata Sh. 15,000 hadi 20,000."

"Kwa sasa ukienda sokoni na migebuka ya Sh. 40,000 ni ngumu kuimaliza yote na hali ya maisha inazidi kuwa ngumu kwa kuwa wanategemea ziwa hilo kuendesha maisha yao, kuna kipindi cha nyuma muda huu (asubuhi) walienda kuvua wamesharudi na mzigo mwingi nasi tuna uhakika wa kuuza siku hiyo," alifafanua.

Mfanyabiashara wa siku nyingi wa samaki, Dinna Jackson, biashara hiyo imemsaidia kuendesha familia kwa kuwa amesomesha watoto wake kupitia kazi hiyo.

"Kwa sasa mzunguko wa biashara ni mgumu sana kwa kipato cha wavuvi anaweza kuvua na kupata samaki mmoja au wawili, yaani imekuwa ngumu mno, maji ni mengi sana," anasema.

Anasema mazingira ya samaki yalikuwa mazuri kwa kuwa aliweza kuvuka kwa miguu kwenda kuwatafuta, lakini kwa sasa ni ngumu kupata hata wachache, huku eneo la mwalo walilokuwa wanatumia likijaa maji na hawana eneo rasmi la biashara. "Unapopata Sh. 2,000 unanunua chakula cha familia, unavumilia hivyo hivyo huwezi kujiua, ukipata sawa ukikosa mnalala njaa sawa, kwa kuwa kipato kimekuwa kigumu, kazi nyingine hatuna wenzetu wamezoea kufuma mashuka, lakini sisi kazi yetu ni samaki maisha yangu yote yanategemea Ziwa Tanganyika na sasa kina cha maji kimeongezeka siwezi kupata samaki kama zamani," anasema.

"Baadhi yetu watoto wetu hawajaenda shule kwa sababu fedha hakuna, kule shule hawataki maneno kinachotakiwa ni fedha, mtoto anatakiwa awe na madaftari, viatu, begi ulipie baadhi ya vitu. Usipokuwa na fedha mtoto atakaa nyumbani hadi vifaa vienee unakwenda shuleni kuwaeleza kuwa sijafanikisha kutokana na hali ngumu ya fedha na nikipata atakuja shule," anasema.

Naye Zabibu Hamis anasema baada ya maji kujaa mabwawa ya samaki aina ya ngege yaliharibika na wakarudi ziwani huku wafanyabiashara wakihamishwa eneo hilo kwenda jingine.

Anasema wakiwa kwenye mwalo huo walicheza michezo ya kupeana fedha ili kukuza mtaji, walisaidiana kwa umoja wao, walianzisha vikundi ambavyo vyote vilitawanyika kidogo kidogo kutokana na eneo kujaa maji.

Anasema walikaa zaidi ya miezi sita bila shughuli ya kufanya na kwamba walisambaa sehemu mbalimbali kila mmoja akienda kutafuta maisha kwingine.

"Mitaji ilishuka, huingizi fedha unatoa tu mwishowe unakula hadi mtaji, wengine walienda kulima mihogo na nyinginezo, kuna watoto wameshindwa kwenda shule maana huwezi kumpeleka bila viatu na sare za shule," anasema.

Anasema waliingia kwenye biashara ambayo hawakuitegemea ambayo haiwaingizii kipato kama ya samaki, lakini hawana cha kufanya kwa kuwa wanahitaji kupata kipato ili kutosheleza mahitaji ya familia.

**Ripoti Maalum hii imefadhiliwa na Chama cha Wachapishaji wa Habari Duniani (WAN-IFRA) kupitia Social Reporting Initiative (SIRI).**

# MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

**Imethibitishwa na ISO 9001: 2015**

## TAARIFA KWA UMMA KUHUSU
## WAJIBU WA KUDAI RISITI ZA EFD KWA WANUNUZI WA BIDHAA AU HUDUMA

**Dar es Salaam, Januari 21, 2022:**

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) inapenda kuwakumbusha wanunuzi wote wa bidhaa au huduma kuhakikisha wanadai risiti za EFD pale wanapofanya manunuzi ili kutimiza wajibu wao wa kisheria. Aidha, wanunuzi wote wa bidhaa au huduma wanakumbushwa kuhakikisha thamani iliyo kwenye risiti ni sawa na kiasi cha fedha walicholipa au wanachotakiwa kulipa.

**Kifungu cha 36 cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi, SURA 438** kinatoa wajibu kwa muuzaji wa bidhaa au huduma kutoa risiti ya EFD pindi anapofanya mauzo na vilevile **Kanuni ya 55(1) ya Kanuni za Usimamizi wa Kodi ya Mwaka, 2016** inampa wajibu mnunuzi wa bidhaa au huduma kudai risiti pale anapofanya manunuzi na kuionyesha kwa Kamishna au Afisa wa Kodi pindi anapotakiwa kufanya hivyo.

Ni kosa kisheria kwa mnunuzi yeyote kutokudai risiti pindi anaponunua huduma au bidhaa. Kwa mujibu wa **Kifungu cha 86(4) cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi, SURA 438**, mnunuzi atakayebainika kutodai risiti atawajibika kulipa faini isiyopungua **TZS 30,000** na isiyozidi **TZS 1,500,000** kama adhabu.

Hivyo wanunuzi wote wa bidhaa au huduma wanakumbushwa kuendelea kudai risiti za EFD na iwapo muuzaji wa huduma hiyo au bidhaa hatampatia risiti, mnunuzi anatakiwa kutoa taarifa katika Ofisi za TRA zilizopo jirani naye kama inavyoelekezwa kupitia **Kanuni ya 55(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Kodi ya Mwaka, 2016** au kupiga simu kupitia namba ya bure ya huduma na elimu kwa mlipakodi ambazo ni **0800 750 075 au 0800 780 078**.

Kuanzia tarehe **01/02/2022** TRA itafanya operesheni maalumu za ukaguzi wa risiti za manunuzi ya bidhaa na huduma katika maeneo mbalimbali nchi nzima ikilenga kuhakikisha kila mnunuzi anatimiza wajibu wake wa kisheria kwa kudai risiti pale anapofanya manunuzi.

***Epuka usumbufu, ukiuza toa risiti na ukinunua dai risti.***

***"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"***

Imetolewa na;

**A.J Kidata**
**KAMISHNA MKUU**
**MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA**

216662702

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Waamuzi bado kikwazo ushindani Ligi Kuu nchini

**KADRI** muda unavyozidi kusonga mbele Ligi Kuu Bara inazidi kuwa ngumu, lakini na kuwa kivutio kikubwa kwa watazamaji na si Tanzania pekee, bali katika ukanda huu wa Afrika Mashariki na Kati na imeonyesha wazi inastahili kabisa kushika nafasi ya nane kwa ubora barani Afrika.

Kwa sababu hiyo hatutachoka kulipongeza Shirikisho la Soka nchini (TFF), Bodi ya Ligi (TPLB), wadau wote wa soka hususan wadhamini kuanzia wale wa ngazi ya klabu hadi wa ligi hiyo pamoja na mashabiki wote kwa kuunga mkono juhudi hizo.

Ni wazi TFF na TPLB wametumia na kubwa kuwashawishi wadhamini hadi kuandika historia kwa mara ya kwanza tangu ligi hiyo kuanzishwa nchini kuwapo kwa wadhamini wakubwa zaidi ya watatu waliokubali kudhamini Ligi Kuu kwa mabilioni ya shilingi.

Na taratibu sasa mashabiki wa soka nchini wanaonekana kuvutiwa zaidi kutazama mechi za Ligi Kuu nchini na kusahau ligi pendwa duniani ya kama England, Hispania, Italia, Ujerumani na Ufaransa au wakati mwingine inapolazimu huangalia zote kwa pamoja, hakika si kazi ya mchezo iliyofanywa katika kuiboresha na kuwa na mvuto.

Lakini hilo limechangia pia kuwavutia wageni wengi kuja kucheza soka nchini, na si Ligi Kuu tu bali hata Ligi Daraja la Kwanza (Championship) kwa sasa wamesajiliwa huko na kuongeza ushindani na viwango vya wachezaji wazawa.

Kutokana na uwapo wa wageni kumesaidia kwa asilimia kubwa kuongezeka kwa ubora wa wachezaji wazawa jambo ambalo litakwenda kuongeza kitu katika timu zetu za taifa, kuanzia zile za vijana hadi wakubwa, Taifa Stars.

Hiyo ni kutokana na wachezaji wetu wengi wanaunda timu za taifa kucheza soka la ndani, jambo ambalo halitoi fursa kwao kuweza kujifunza mbinu nyingi kutoka kwa wachezaji wenzao ama makocha wa kigeni.

Na katika hilo, pia tumeshuhudia zaidi ya asilimia 90 ya timu zinazoshiriki Ligi Kuu Bara zikinolewa na makocha wa kigeni, kitu ambacho pia kinatoa fursa kwa wachezaji wetu wazawa kujifunza mambo mengi, hivyo tunaamini huu ni mwanzo wa kupata matokeo chanya kwa timu zetu za taifa.

Uwapo wa wachezaji kutoka Senegal, Mali, Ivory Coast na makocha kutoka Tunisia, Hispania, Brazil na Afrika Kusini ni wazi kuna kitu wachezaji wazawa watanufaika nacho hususan kimbinu na kiufundi, hivyo ni wakati wa kuzidi kuhamasisha wageni zaidi kuja kufanya kazi nchini.

Wanaoweza kuongeza ama kuua kabisa hamasa hiyo kwa sasa ni waamuzi, ambao baadhi yao suala la kuchezesha soka kwa kufuata sheria 17 za soka duniani, limekuwa tatizo kubwa kwao, jambo ambalo linazua malalamiko kila wiki.

Kushindwa kumudu mchezo, kufanya kwa makusudi au kwa mapenzi binafsi ama pengine kwa kurubuniwa, kumekuwa kukiathiri sana mechi na kulitia doa soka letu, kitu ambacho tunaona kinaweza kuchangia kwa asilimia kubwa kudidimiza ukuaji na uwekezaji mkubwa ambao umeanza kufanywa na wadau wa soka.

Katika hilo, pia baadhi ya waamuzi wameshindwa kabisa kulinda afya za wachezaji uwanjani kwa kuachia rafu mbaya kuendelea mchezoni kitu ambacho tunaona kama wakiachwa bila kuchukuliwa hatua msimu huu unaweza usimalizike salama.

Hivyo, tunaona ipo haja sasa kwa TFF na TPLB, kutokawia kutoa adhabu kali kwa waamuzi kwa mujibu wa kanuni, ili kulinda ubora wa ligi yetu na kuzidi kuvutia wageni kuja kufanya kazi nchini, lakini wawezekezaji kwa maendeleo ya soka letu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Mastraika wazawa jifunzeni kwa Mayele, Kagere

Na Adam Fungamwango

**UNAKWENDA** uwanjani kutazama mechi hadi inakwisha huoni mashuti, au kashikashi za mastraika kutaka kufunga, badala yake unachoshuhudia wanagombana na kuminyana na mabeki tu, wakitoleana maneno makali.

Hao ndiyo mastraika wengi wa Kitanzania na ndiyo maana hadi leo hii ni zaidi ya miaka mitano sasa, kwenye kikosi cha timu ya Taifa, Taifa Stars bado wanategemewa Mbwana Samatta na Simon Msuva kufunga mabao.

Mastraika wengi wa Kitanzania ni maji kupwa kujaa. Leo anaweza kucheza vizuri, lakini kesho ukashangaa kama ni yule yule au mwingine. Wakati mwingine wanakuwa na wachezaji wa msimu tu.

Msimu huu anaweza kufunga hata mabao 12, lakini ujao asiwe na mwendelezo. Akashindwa hata kufikisha mabao saba. Tumewaona huko nyuma wachezaji kama kina Abdulrahman Mussa, Salum Aiye, Adam Adam, Waziri Junior, Yusuph Mhilu, Habib Kyombo, Eliud Ambukile, Mohamed Rashid, Marcel Kaheza, na wengine wengi wakifanya vema kwa kutupia mabao kwenye misimu tofauti, lakini cha ajabu wakashindwa kufanya tena kama hivyo misimu iliyofuata na kubaki kuwa ni wachezaji wa kawaida tu. Na wala hawakuweza kuwashawishi walimu wa Taifa Stars kuwaita kwenye kikosi hicho.

Ni John Bocco pekee ambaye ameweza kucheza Ligi Kuu misimu 13 mfululizo tangu 2008/09, akiwa na wastani wa kufunga mabao 10 kila msimu. Ndiye straika pekee wa Kibongo aliyedumu kwa kiwango chake kwa muda mrefu. Hata kama kwa sasa kiwango chake kimepungua, lakini ni kama hadaiwi na mtu, amecheza kwa muda mrefu mno na kwa mafanikio makubwa uwanjani kuliko mwingine yeyote yule. Wengine alioanza nao wameshaacha kucheza soka la ushindani. Na waliomkuta, wamebaki kuwa wachezaji wa kawaida tu kuliko yeye. Sifa ya straika ni kufunga, na anatakiwa aone aibu kutoka uwanjani bila bao. Iwe bahati mbaya kwa mechi moja, lakini mastraika wa Kitanzania wanaweza kucheza hata mechi tano mpaka nane bila bao. Tatizo ni nini? Tatizo kubwa ni mikimbio wakiwa uwanjani. Mastraika wengi wa Kitanzania wanacheza uwanjani kama vile kuna kitu wanawaza nje ya uwanja. Wanaamua cha kufanya wakati mpira umeshafika, wengi hawajui kuruka vichwa, pia ugonjwa mwingine ni kutokuwa na uwezo wa kupiga mashuti.

Zamani sifa namba moja ya straika ni kuweza kupiga mashuti ya mbali, kama huna basi huwezi kuwa straika.

Zamoyoni Mogella, mmoja wa mastarika hatari wa Tanzania aliyewahi kutokea, aliyecheza kwa mafanikio makubwa akiwa Simba na kumalizia msimu mmoja klabu ya Yanga, anasema straika unakuwa kitandani usiku, kabla hujapata usingizi ni lazima utengeneze mpango mkakati wa kufanya ili uweze kufunga mabao. "Utakabwa sana na mabeki, lakini utatafuta njia mbalimbali, utakimbia huku na huku ukiwatoroka, lakini nafasi yoyote itakayopatikana ni lazima itumike ipasavyo," anasema. Ndiyo maana alikuwa na uwezo wa kufunga kwenye mazingira yoyote yale, nje ya boksi, ndani, pembeni, na ameshawahi kufunga hata katikati ya uwanja kwenye mechi moja dhidi ya Majimaji ya Songea.

Ukiwaangalia mastraika wa sasa, Fiston Mayele wa Yanga na Meddie Kagere wa Simba unapata picha ya kina Mogella. Kwa bahati mbaya sana wote si Watanzania. Ni watu ambao wanajua kwenda na 'muvi' ya mpira. Mastraika wengi wamwangalia Mayele. Si mvivu, krosi ikipigwa yeye tayari yupo golini na atatia kashikashi ili tu aonekane yupo. Mabeki wa timu pinzani wanakuwa muda wote wapo makini naye. Hii ndiyo sifa ya straika, beki anapoukosa mpira wa krosi, basi tabu itamkuta. Leo hii mastraika wetu, zinapigwa krosi hata kumi na zinawapita mabeki, lakini hawapo kwenye eneo husika.

Mayele anafunga mabao kutokana na kujua maeneo ya kukaa pamoja na uchu wa kufunga. Kipa wa Yanga, Djigui Diarra baada ya mechi dhidi ya Simba, alisema kuwa mtu aliyekuwa anamhofia kuwa wakati wowote wanaweza akamfunga ni Kagere kwa sababu ya kukaa maeneo ambayo anadai ni ya hatari sana kama angekuwa anapata mpira kutoka kwa wenzake.

Akasema yeye kama kipa wa kimataifa na mzoefu anajua maeneo ambayo straika yupo kwenye eneo ambalo akipata mpira inakuwa hatari sana. Hivyo, mastraika wa Kibongo hebu tafuteni video za hao ili msome mikimbio yao, inaweza kuwasaidia sana ni ushauri tu!

# Wizara, NMB kuendeleza utalii Zanzibar

**Na Mwandishi Wetu**

WIZARA ya Utalii na Mambo ya Kale ya Zanzibar imeweka mikakati ya kushirikiana na Benki ya NMB kutoa mafunzo kwa vijana wanaotembeza watalii ili kurasimisha shughuli zao waweze kukopesheka.

Hayo yameelezwa jana na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Fatma Mabrouk Khamis, wakati wa kutiliana saini makubaliano kati ya wizara hiyo na Benki ya NMB kuinua shughuli za utalii visiwani humo.

Akizungumza wakati wa mkutano huo uliofanyika jana visiwani Zanzibar, Fatma alisema kuna kundi kubwa la vijana wanaozagaa mitaani bila ujuzi wa kuongoza watalii, ambao wanaharibu taswira ya visiwa hivyo, ambapo wakipewa mafunzo na kurasimishwa itawasaidia kiuchumi na kijamii.

"Vijana wanaojihusisha na utalii mfano beach boys ambao mara nyingi wanakuwa kero kwa wageni, wanafanya utalii wa mikobani. Kwa kushirikiana na NMB tutawakusanya tutawapa mafunzo na kuangalia ni kwa namna gani tunaweza kuwaunga na jumuiya ili kuwahusisha na kuwarasimisha na kuwaongoza, hakuna mikakati inayowasimamia," alisema Bi Fatma.

Alibainisha kuwa mpango wa kuboresha mashamba ya viungo, ambapo kuna vijana wanajihusisha na shughuli hizo: "Tutashirikiana na NMB kuwapa mafunzo na mikopo ili kuboresha bidhaa zao, tutawashika mkono ili kuhakikisha wanatoa huduma nzuri na bidhaa nzuri. "Spice Tour haina viwango vinavyostahiki, pia wizara ina mkakati wa kuanza kuhusisha vijiji kuwe na Village Tourism ili kulinda utamaduni wetu. Hivi karibuni tulikwenda Pemba kukagua miradi yetu ili kuiendeleza zaidi na kuangalia namna gani vijana wanaweza kunufaika."

Ofisa Mkuu wa Biashara na Wateja Binafsi wa Benki ya NMB, Filbert Mponzi, alisema benki hiyo imekuwa ikifanya mambo mengi makubwa visiwani Zanzibar kwa lengo la kuinua sekta ya utalii, ndiyo maana wameamua kupeleka vituo vya mauzo 100 (Point of Sales) ambapo kwa sasa wanaomba Wizara ya Utalii kuwaelekeza vituo watakaposambaza vifaa kwa ajili ya kufanyia malipo.

"NMB ndio benki kubwa zaidi nchini ambayo serikali ni mdau mkubwa, lakini inaongoza kwa kupata faida yaani kwa ukubwa, tunapoingia kwenye jukumu kama hili hatuna wasiwasi," alisema Mponzi na kuongeza:

"Tumeshiriki katika mambo ya huduma kwa jamii mbalimbali hapa Zanzibar, tunatoa sana nchi nzima hakuna makubaliano tunayoingia bali tunasaidia kwa wenye uhitaji. Kama tumeamua kujifunga kwa Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale Zanzibar maana yake tutafanya kitu kikubwa katika utalii Zanzibar."

Awali, Mponzi alisema katika safari hii ya kuimarisha uchumi wa bluu na kwenda sambamba na dunia kukuza uchumi kupitia mifumo ya kidigitali, NMB imekubaliana na Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale mambo kadhaa.

Miongoni mwake ni kutoa elimu na kuhamasisha watu kuzidi kutembelea vivutio vya kitalii vilivyoko Zanzibar kupitia matamasha na promosheni mbalimbali.

Pia kuchagiza shughuli za kitalii Zanzibar kwa kuwekeza kwenye mfumo wa kidigitali zaidi utakaotumika katika makusanyo ya serikali katika vituo vyote vya utalii Zanzibar.

Kadhalika, kusambaza mashine za malipo yaani POS kwenye vituo vya makusanyo na vivutio vya utalii. Hii itawawezesha watalii kulipia ada na tozo zote kupitia kadi zao za Mastercard, Visa na UnionPay.

Aidha, kuongeza idadi ya POS katika maeneo ya hoteli, migahawa, sehemu za starehe na maduka ilikuruhusu malipo kupitia kadi. Hii itapunguza ulazima wa watalii kutembea na fedha taslimu, hivyo kuwawezesha kufanya malipo kwa njia salama na rahisi.

# Walioshtakiwa kwa kulima bangi waachiwa huru

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi, imewaachia huru washtakiwa wawili waliokuwa wanadaiwa kulima bangi na kukutwa nayo kilo 4492.43 baada ya kujiridhisha upande wa Jamhuri umeshindwa kuthibitisha mashtaka bila kuacha shaka.

Hukumu hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki mbele ya Jaji Immaculate Banzi, baada ya kupitia ushahidi wa mashahidi watano wa upande wa Jamhuri na utetezi wa washtakiwa.

Washtakiwa katika kesi hiyo, Hamisi Selemani na Msailo Msailo, wanadaiwa Novemba 13, 2016 katika Kijiji cha Kwala Kibaha, walishtakiwa kwa kusafirisha dawa za kulevya aina ya bangi kilo 4492.43.

Akisoma hukumu hiyo alisema mahakama ilizingatia kwa makini ushahidi wa pande zote mbili pamoja na vielelezo vilivyotolewa mahakamani.

Alisema katika ushahidi wa upande wa mashtaka hakuna uthibitisho nyumba iliyokutwa na bangi inamilikiwa na mshtakiwa wa pili.

"Kwa mujibu wa ushahidi wa utetezi wa mshtakiwa wa pili nyumba hiyo mali ya Saidi Ulata, iko umbali wa dakika 30 kwa kutembea kutoka eneo la tukio hadi ilipo na mshtakiwa wa pili anaishi kwenye kachumba kadogo sio nyumba.

"Mkanganyiko huo unaleta mashaka katika ushahidi wa shahidi wa kwanza, shahidi wa kwanza anasema bangi ilikutwa kwenye dari wakati shahidi wa tano anadai kwenye darini hakukuwa na kitu," alisema Jaji.

Alisema mashahidi hao wawili, mmoja anadai pikipiki sita na pampu za maji sita zilikutwa kwenye chumba cha nje wakati mwingine anadai hakukuwa na chumba cha nje.

Jaji Banzi alisema upande wa Jamhuri hawakuleta shahidi wa kuthibitisha nani kati ya washtakiwa au mtu mwingine ni mmiliki wa pikipiki hizo.

Alisema upande wa Jamhuri haujathibitisha nani kati ya washtakiwa ni mmiliki wa nyumba inayodaiwa kukutwa na pikipiki hizo.

"Washtakiwa katika ushahidi wao wa utetezi wanadai pikipiki hizo zilikusanywa katika nyumba mbalimbali ambazo wahusika walikimbia.

"Ushahidi wa Jamhuri una mashaka mengi na inapokuwa hivyo anayenufaika ni mshtakiwa, mahakama inaona upande wa Jamhuri umeshindwa kuthibitisha kesi dhidi ya washtakiwa bila kuacha shaka yoyote.

"Mahakama hii inaamuru kuondoa mashtaka dhidi ya washtakiwa na waachiwe huru," alisema Jaji Banzi.

Katika kesi hiyo upande wa Jamhuri uliwakilishwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Kasana Maziku, akisaidiana na Wakili wa Serikali, Elizabeth Mkunde na Edith Mauye.

Ushahidi wa Jamhuri inadaiwa walipata taarifa kuna watu maeneo ya Kipera Kwala, wanajihusisha kulima bangi na kusafirisha maeneo ya mjini kwa kutumia pikipiki.


## NATIONAL INVESTMENTS PLC

NICOL

The Economic Shield of the Nation

## APPOINTMENT OF INDEPENDENT NON-EXECUTIVE DIRECTORS

The National Investments Plc (NICOL) is a public listed company at the Dar-Es-Salaam Stock Exchange (DSE), whose mission is to promote active participation of Tanzanians in the national economy, by utilizing investment resources derived both locally and internationally.

As a measure of NICOL`s dedicated efforts to build on contemporary achievements and notable success in its investment portfolios, the company looks beyond the horizon with an ambitious expansion program towards unlocking long-term values driven by sustainable growth, compatible high level professional acumen and international best practices, upholding well established principles of integrity and governance. With that in mind, coupled with expansion projections entailing investment diversification beyond the equity market, the Annual General Meting of the Shareholders of NICOL, which took place on 3rd December 2021, approved a Recommendation to increase the size of the Board to seven (7) Directors, which gives opportunity for appointment of four (4) additional Directors, commensurate with the rapid expansion of the company`s business activities, and the recent increase in shareholder`s value and profits.

**Duties and Responsibilities:**

1. Formulating and Embellishing NICOL's Vision, Mission, Objectives as well as Apprising its Strategy by Ensuring that the Company Survives and Thrives as an On-gong Concern.
2. Developing, Promoting and Monitoring the Implementation of NICOL`s Strategic Objectives, Plans and Structures.
3. Ensuring Observance of Regulatory Compliance and Good Corporate Governance Practices.
4. Carrying out Basic Board Responsibilities, including Appointment of Senior Executives of NICOL, as well as Overseeing, Reviewing and Evaluating Board and Management performance.
5. Keeping Abreast with NICOL`s Activities by Regularly Attending Board and other Meetings and Actively Participating in Policy and Performance Assessment / Evaluation and Planning For a and Volunteering to Undertake Board Assignments.
6. Enhancing an Amicable Working Relationship with Other Board Members.

**Requirements:**

(a) Multiskilled with experience in finance, economics, investments and legal
(b) Holder of a Degree from a Recognized University.
(c) Possessing Knowledge in Good Corporate Governance Practices.
(d) Having Minimum Experience of Five Years as Board Director of a Major Company.
(e) Possessing High Moral and Ethical Character, Unblemished by any Criminal Record Or History of Bankruptcy.

**National Investments PLC (NICOL)** is an equal opportunities employer and is committed to promoting equality and diversity in the workplace. Applications are encouraged from all representative groups. Applications will be considered and appointments made solely on merit.

All applications should be marked **"APPLICATION FOR INDEPENDENT NON – EXECUTIVE DIRECTOR"** on top of an envelope and submitted to NICOL by Post or Courier (EMS, CUM, DHL) to the following address.

**Chief Executive Officer,**
**National Investments Plc,**
**3rd Floor, Mirambo House,**
**50 Mirambo Street,**
**P.O. Box 7465,**
**Dar-Es-Salaam.**

Online applications are preferred with a cover letter quoting reference **NICOL INDEPENDENT NON -EXECUTIVE DIRECTOR to invest@nicol.co.tz**. For more information please contact us through our email **invest@nicol.co.tz or on 022 2111 399**.

**THE DEADLINE FOR SUBMISSION OF APPLICATIONS IS 7th FEBRUARY 2022 AT 15:30 HOURS.**

216661702

# Diwani aangua kilio barazani kisa adha ya mamba, viboko

**Na Gurian Adolf,** NKASI

DIWANI wa Kizumbi Wilaya ya Nkasi mkoani Rukwa, Oswald Kamsipi, ameangua kilio katika kikao cha madiwani akiiomba halmashauri iwapeleke maofisa maliasili ili wawaue mamba na viboko wanaozagaa katika vijiji vya kata hiyo na kusababisha vifo na kuwajeruhi wananchi.

Tukio hilo lilitokea mwishoni mwa wiki wakati Baraza la Madiwani limeketi kwa ajili ya kikao cha robo ya pili ya mwaka muda, ambao kamati ya uchumi, ujenzi na mazingira ikiwasilisha taarifa yake na diwani huyo kupata nafasi ya kuuliza swali.

Alisema kuwa kwa muda mrefu amekuwa akiiomba halmashauri hiyo itume watendaji wa idara ya maliasili ili wakawaue kwa kuwapiga risasi mamba na viboko waliotoka mtoni na ziwani, ambao wamehamia vijijini na wamekuwa wakiwaua wananchi, kuwajeruhi pamoja na kula mazao, lakini ombi lake limekuwa halipewi umuhimu.

"Mheshiwa mwenyekiti, kila mara nimekuwa nikiomba watu wa idara ya maliasili waje kwenye kata yangu pamoja na kata nyingine zilizoko mwambao mwa Ziwa Tanganyika wawaue viboko na mamba ambao wanatoka ziwani na mitoni... hivi sasa wamehamia vijijini, tunaishi nao kama nao wana nyumba katika vijiji vyetu," alisema.

"Katika kipindi cha Januari mwaka 2021 mpaka Januari mwaka huu, watu 11 wamekufa kwa kuliwa na mamba na viboko, watu wanane wamejeruhiwa, wengine wanajiuguza majeraha hayo mpaka sasa... mnataka mimi niwaombeje jamani?" Alihoji Kamsipi, huku akitokwa na machozi.

Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira, Everist Mpemba, alisema kuwa msimamo wa kamati hiyo ni kutaka mamba na viboko hao wauawe, kwani wamekuwa ni tishio kwa maisha ya wananchi, na kwamba kamati ina taarifa ya vifo na majeraha waliyoyapata wananchi hao yaliyotokana na wanyama hao.

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Pankras Maliyatabu, alisema halmashauri hiyo imekisikia kilio cha diwani huyo pamoja na madiwani wengine ambao kata zao zinapakana na Ziwa Tanganyika, kwani wamekuwa na kilio sawa na hicho na kumtaka diwani huyo afute machozi kwa kuwa amesikika.

Alisema hata katika bajeti ya Mwaka wa Fedha wa 2022/2023, halmashauri imeongeza fedha katika bajeti ya kununua risasi, lengo likiwa kuwaua mamba na viboko hao kwa kuwa wanasababisha vifo kwa wananchi, hivyo halmashauri haiwezi kuyaweka rehani maisha ya wananchi.



Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ambaye ni Mbunge wa Jimbo la Chalinze mkoa wa Pwani, Ridhiwani Kikwete, akiangalia moja ya nyumba iliyoathirika na mvua katika kijiji cha Makombe, Chalinze mkoani Pwani alipokwenda kutoa pole na kujionea athari za mvua mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Askofu awakumbusha Watanzania kudumisha amani

**Na Paulina Chimeledya, TUDARCo**

ASKOFU wa Jimbo la Iringa, Tarcisius Ngalalekumtwa, amewataka Watanzania kudumisha amani na kuwekeza kwenye elimu ili kuendelea kuandaa wataalamu wa fani mbalimbali nchini. Akihubiri wakati wa ibada ya Misa Takatifu katika Kanisa Kuu la Moyo Mtakatifu wa Yesu, Parokia ya Kihesa, Jimbo la Iringa, alisema ni muhimu wananchi wakafundishwa elimu ya mema ambayo Mungu anatamani na kutarajia binadamu wayatende kila siku.

"Ili amani ya kweli iwepo lazima kuwe na somo la kudumu ambalo ni elimu, tujitahidi kukuza na kuwekeza kwenye elimu, siku hadi siku mataifa mengi duniani wanawekeza kwa ajili ya silaha za kivita, ili amani iwepo tujitahidi kuwekeza kwenye elimu kutuliza moyo kuliko silaha hizo," alisema.

Alisema kwenye maandiko amani ni tunda la haki kila mmoja anapomjali mwenzake na kumwachia nafasi aliyopewa na Mungu aishike yeye bila kusababisha malumbano na kila mtu kujisikia kuthaminiwa.

"Papa Francis anataja maeneo matatu ambayo ndani yake amani ya kweli inaweza kujengwa, anasema ili kuwe na amani ya uhakika ni lazima tuwe ni watu ambao tunazungumza kati ya kizazi kimoja na kingine ili kuleta maelewano na ushirikiano, kizazi kinachotangulia kinarithisha mema kwa wale wanaofuata, hawa wanaotangulia wawape nafasi wanaofuata ili kukuza karama zao," alisema.

# Kujifungulia nyumbani kutozwa faini 50,000/-

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

VIJIJI sita katika kata ya Ubagwe Halmashauri ya Ushetu mkoani Shinyanga, vimeweka utaratibu wa kumtoza faini ya Sh. 50,000 mjamzito atakayebainika kujifungulia nyumbani badala ya zahanati ama kituo cha afya.

Utaratibu huo unalenga kuwalazimisha wajawazito kwenda vituo vya afya ama zahanati kujifungua, badala ya kujifungulia nyumbani ili kuepukana na vifo vinavyoweza kutokea kutokana na kukosa wataalamu wa afya.

Faini hiyo hutozwa baada ya mjamzito kujifungulia nyumbani na kuzalishwa na watu wasiokuwa na ujuzi wakufanya kazi hiyo.

Wajawazito katika vijiji hivyo walikuwa wanalazimika kujifungulia nyumbani, licha ya kuwapo faini hiyo kutokana na zahanati waliyokuwa wakiitegemea kuwa umbali wa kiliomita 15.

Kutokana na hali hiyo, mjamzito alikuwa analazimika kutembea umbali wa kilomita 30 kufuata huduma za afya katika zahanati iliyoko makao makuu ya kata.

Kampuni ya ununuzi wa zao la tumbaku ya JTI iliamua kuingilia kati ya kujenga zahanati katika vijiji hivyo ili kuwapunguzia wajawazito mwendo mrefu kufuata huduma za afya.

Zahanati iliyojengwa na kampuni hiyo imegharimu Sh. milioni 289.13, ili kuhakikisha huduma za afya hususani kwa wajawazito zinakuwa jirani na wananchi.

Baadhi ya wananchi wa kata hiyo wakizungumza na Nipashe, walishukuru kampuni hiyo na kuongeza kuwa itasaidia kuondoa kero iliyokuwapo ya kutembea umbali mrefu kufuata huduma za afya.

Hafla ya uzinduzi wa zahanati mpya iliyojengwa na kampuni hiyo ilihudhuriwa na Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Festo Kiswaga na Mbunge wa Ushetu, Emmanuel Cherehani pamoja na wataalumu kutoka Ofisi ya Mkurugenzi wa Ushetu.

Mkazi wa kijiji cha Ilamba, Joyce Charlea alisema, kabla ya kujengwa kwa zahanati hiyo wajawazito walilazimika kutembea umbali wa km 30 kwenda na kurudi kliniki katika zahanati ya Ubagwe na walipojifungulia nyumbani kijiji kiliwatoza faini ya Sh. 50,000.

Mganga Mfawidhi wa Zahanati ya Ubagwe, Dk. Nashoni Ndakazi, alisema kukamilika kwa zahanati hiyo kutasaidia kupunguza msongamano wa wagonjwa kwao kwa kuwa walikuwa wanapokea 30 hadi 40 na asilimia kubwa ni wanawake, watoto na wajawazito wanaofika kujua hali ya mtoto tumboni.

Akitoa taarifa ya ujenzi wa zahanati hiyo mpya, Meneja wa JTI kanda ya Ulyankulu na Ulowa, Joramu Kissia, alisema, Sh. milioni 289.1 zilitumika.

Aidha, alisema wametoa vifaa tiba vya kuanzia kutoa huduma kwa wananchi vyenye thamani ya Sh. milioni 49.9, madawati 300 kwa ajili ya shule za msingi na sekondari vilivyogharimu Sh. milioni 37.5 na uchimbaji wa mabwawa 8 kwa Sh. milioni 151 kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji wa mboga na tumbaku.

# Kibano kwa viwanda bubu vya dawa za mifugo

**Na Mbaraka Kambona**

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, amesema serikali inaendeleza jitihada za kudhibiti utengenezaji holela wa dawa za mifugo na zisizokidhi viwango za mifugo zinazoingizwa, ili kuwalinda wafugaji nchini.

Waziri Ndaki alibainisha hayo jana alipotembelea eneo la Kampuni ya Uzalishaji, Usambazaji na Uingizaji wa pembejeo za mifugo na Kilimo (Farmbase) lililoko wilayani Kigamboni, mkoani Dar es Salaam ambalo wanataka kujenga kiwanda kikubwa cha kuzalisha dawa za mifugo.

Alisema kumekuwa na malalamiko kutoka kwa wafugaji kuwa kuna baadhi ya dawa wanazozitumia kutibu mifugo yao haziwapi matokeo wanayoyatarajia, na ndio maana serikali inaendelea kudhibiti uuzwaji holela wa dawa hizo na kuimarisha utaratibu mzuri wa kupatikana dawa halisi za mifugo.

"Hivi karibuni tuna mpango wa kuweka maduka ya kuuza dawa katika kila mnada ili kuwahakikishia wafugaji wetu kwamba dawa aliyonunua kutoka katika maduka hayo ni sahihi kuitumia, mpango wetu haya maduka yaendeshwe na watu binafsi chini ya usimamizi wa serikali," alisema Ndaki

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Farmbase, Suleiman Msellem, alisema kuwa wao wapo tayari kushirikiana na serikali katika kuhakikisha dawa halisi kwa ajili ya mifugo zinapatikana kwa wingi nchini.

"Njia moja ya kuondosha dawa feki ni kupatikana kwa dawa halisi, sisi tupo tayari kushirikiana na serikali yetu, na hata hayo maduka yakianzishwa tupo tayari kushirikiana katika kuzisambaza dawa kwenye maduka hayo," alisema Msellem.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu, Dk. Pindi Chana, akizungumza na Baraza la Wazee wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Dodoma Mjini, alipofanya ziara ya kutembelea ujenzi wa mji wa serikali ulioko Mtumba jijini Dodoma. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Benki ya Stanbic yazindua upya tawi lake la Kariakoo

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Stanbic Tanzania imefungua upya tawi lake la Kariakoo kufuatia janga la moto lililotokea katika soko la Kariakoo ambapo tawi la zamani liliathiriwa.

Taarifa ya benki hiyo ilieleza kuwa tawi jipya sasa lipo Plot no 24, Block "56", Narung'ombe/Sikukuu Street, Kariakoo.

Hafla ya uzinduzi huo ilihudhuriwa na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, akiwa mgeni rasmi ambapo Mtendaji Mkuu wa Benki ya Stanbic Tanzania, Kevin Wingfield, akizungumza kwenye uzinduzi huo, alisema hatua hiyo ya kimkakati inalenga kuendelea kuwahudumia wafanyabiashara walioko Kariakoo na maeneo ya jirani.

"Tawi letu la Kariakoo limekuwapo kwa zaidi ya miaka 10. Tumechagua kubaki eneo la Kariakoo kwa sababu tunafahamu umuhimu wa mchango wa wafanyabiashara wa Kariakoo kwa uchumi wa Taifa pamoja na nchi jirani."

Wingfield aliongezea kuwa kupitia tawi hili jipya benki itaendelea kushughulika na mahitaji ya kifedha ya wateja wake wakiwamo watu binafsi, wajasiriamali, na biashara.

Kwa upande wake, Makalla aliipongeza Benki ya Stanbic kwa jitihada zao za kuhakikisha wakazi wa Kariakoo wanapata huduma za kifedha kwa urahisi.

Naye Mkuu wa Kitengo cha Wateja wa Rejareja wa Benki ya Stanbic, Omari Mtiga, alisema benki hiyo yenye historia kubwa ya kufanya kazi kwa zaidi ya miaka 25 nchini ina utaalamu na uwezo wa kuchochea uwekezaji ndani ya Tanzania na kukuza uchumi wa Tanzania na jirani.

Mtiga aliongeza kwamba wateja watafurahia ushauri kutoka kwa wataalamu wa masuala ya fedha waliojikita katika kuwasaidia kufanikisha ndoto zao.

# Wajengewa uwezo vita dhidi ya rushwa ya ngono kwa wanafunzi

**Na Sabato Kasika**

JAMII imetakiwa kuheshimu na kulinda haki za watoto, kama njia mojawapo itakayosaidia kukomesha rushwa ya ngono na vitendo vingine vya ukatili ambavyo wamekuwa wakikumbana navyo.

Wito huo ulitolewa juzi na Ofisa Ustawi wa Jamii kutoka Mahakama ya Watoto Kisutu jijini Dar es Salaam, Asha Mbaruku, katika mkutano wa kujengea uwezo wadau wanaopambana na rushwa ya ngono kwa wanafunzi.

Mkutano huo uliandaliwa na Shirika la Wanawake Katika Jitihada za Kimaendeleo (WAJIKI) ambao ulikutanisha wadau mbalimbali wakiwamo madereva wa bodaboda, daladala na bajaj.

Wengine ni walimu, wanafunzi, maofisa wa ustawi wa jamii, TAKUKURU, Polisi na viongozi wa dini, ambapo ofisa huyo alihimiza umuhimu huo ili watoto waweze kuwa salama zaidi.

"Baadhi ya haki za watoto ni kuishi, kupendwa, kushirikishwa katika mambo yanayowahusu, lakini na kusikilizwa. Kwa njia hiyo tunaweza kumaliza mambo ya rushwa ya ngono na kujenga jamii bora," alisema Asha.

Alisema, ili kufanikiwa katika hilo, ushirikiano wa pamoja kati ya wadau unahitajika na kwamba, WAJIKI ni miongoni wale wanaoonyesha mfano katika vita dhidi ya rushwa ya ngono kwa wanafunzi.

Ofisa Mchunguzi Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Kinondoni, Dorothea Mrema, alisema mtu yeyote asitumie nafasi yake kurubuni au kuomba rushwa ya ngono wanafunzi, kwa kuwa kufanya hivyo ni kuwahabilia ndoto zao.

"Madereva wa bodaboda, bajaj na daladala ambao wamekuwa wakituhumiwa kutumia vibaya nafasi zao, wana uwezo wa kuwasafirisha wanafunzi na kuwafikisha salama iwapo watatambua hilo," alisema Dorethea.

Alisema, TAKUKURU ina kaulimbiu ya 'Vunja ukimywa kataa rushwa ya ngono', na kwamba wao kama taasisi, wanaendelea kuikumbusha jamii kuzingatia hilo kuwa rushwa ni adui wa haki.

Mkurugenzi wa WAJIKI, Janeth Mawinza, alisema shirika hilo, limekuwa likipambana na rushwa ya ngono kwa wanafunzi wa kike kwa kushirikiana na baadhi ya madereva wa hao ambao wamejitolea kuwa mabalozi wa vita hiyo.

"Kwa sasa tuna madereva zaidi ya 3,000 katika wilaya za Kinondoni, Ilala na Temeke waliounda vikundi vyao kama 100, ambavyo wanavitumia kuelimisha wenzao kuacha kurubuni wanafunzi wa kike kwa lifti," alisema Janeth.

Alisema wanashirikisha madereva hao katika vita hiyo, kwa madai kwamba ndiyo wamekuwa wakituhumiwa kurubuni wanafunzi kwa lifti kwa lengo la kutaka kufanya nao mahusiano ya kimapenzi.

"Women Fund Tanzania Trust (WFT), wanatufadhili katika vita hii, lakini tunaomba wadau wengine watuunge mkono, ili tuweze kupanua shughuli zetu hadi mikoani, kwani tunaamini huko nako rushwa hii ipo," alisema.

Dereva wa bodaboda, Msafiri Marin, alisema vita ya rushwa ya ngono inaweza kupata ufanisi mkubwa iwapo jamii itabadilika na kurudi kwenye mila za zamani.

"Sisi kama wadau wa WAJIKI, tunafanya kazi yetu vizuri, lakini wakati mwingine tunakutana na vikwazo kutoka hata kwa wazazi na walezi pale tunapoona dereva wa bodaboda tusiyemfahamu akiwa amebeba mwanafunzi, tunaweza kuhoji," alisema Marin.

Alisema, katika mazingira hayo, wakati mwingine kazi yao inakuwa ngumu, na wao wanaamini katika kaulimbiu ya 'Mtoto wa mwenzio ni wako', na kwamba, wakiona mwanafunzi akiwa katika mazingira yasiyoeleweka, wanachukua hatua za kumsaidia, ambapo ameomba wasikwamishwe.

# DC akerwa wanafunzi vyuoni kujiingiza vitendo vya ngono

**Na Friday Simbaya,** IRINGA

MKUU wa Wilaya ya Iringa, Mohamed Hassan Moyo, amesema tabia ya baadhi ya wanafunzi wa vyuo vikuu mkoani Iringa kujihusisha na biashara ya ngono, inadhalilisha utu na hadhi ya vyuo, elimu wanayoipata na hilo si kusudi la serikali.

Akizungumza juzi wakati wa hafla ya kuwakaribisha wanafunzi wa mwaka wa kwanza wa Chuo Kikuu cha Iringa (UOI) zamani kikiitwa Tumaini, alisema serikali imebaini kuwapo kwa wasichana wanaofanya biashara hiyo haramu huku akionya kuwa hatua zitachukuliwa.

Moyo alisema serikali inawategemea wasomi wa elimu ya juu kuwa chachu ya maendeleo kwa kufanya utafiti wenye tija na kuishauri serikali juu ya masuala ya maendeleo na si kujihusisha na vitendo vya aibu.

Alisema tabia hiyo inachafua taswira ya elimu ambayo inatolewa na vyuo vikuu vya mkoani Iringa kwa sababu ya wanafunzi wachache ambao wamejikita katika biashara ya ngono. Moyo alionyesha kukerwa na vitendo vya baadhi ya wanachuo kwa tabia zao za kujihusisha na ngono na kwamba vitendo hivyo vinaondosha thamani au hadhi ya elimu ya vyuo vikuu na kuchafua taswira halisi ya elimu ya juu.

"Ukipita kwenye kumbi mbalimbali za starehe nyakati hasa za usiku, unakutana na wimbi kubwa la baadhi ya wanafunzi wa vyuo vikuu wako wanadanga tu bila sababu yoyote ya msingi, hivyo wanafunzi wenye tabia za aina hiyo, wanatakiwa kuacha mara moja," alisema.

Alisisitiza wanafunzi wa elimu ya juu wanaosoma vyuo mkoani Iringa, kuachana na tabia zisizo na tija na badala yake wajielekeze katika uzalendo wa kweli kwa taifa.

Kwa mujibu wa Moyo, serikali imekuwa inatoa mikopo kwa wanafunzi wa vyuo vikuu ili kuwasaidia kutimiza majukumu yao yaliyowapeleka vyuoni na si fedha hiyo waitumie kwenye starehe kama ambavyo baadhi yao wamekuwa wakifanya.

Moyo alisema hayo kutokana na baadhi ya wanasiasa na wanaharakati kuwatumia vijana wa vyuo vikuu kuichafua serikali kwa kuwakashfu viongozi walioko madarakani na kupinga masuala ya maendeleo pasipo kupima athari zinazoweza kujitokeza kwa taifa.

Alisema kuwa biashara ya ngono ina madhara makubwa kwa wanafunzi kwa kuwa wanaweza kupata mimba na magonjwa mbalimbali ambayo yatasababisha kukatisha ndoto zao za kupata elimu ya juu.

Rais wa Serikali ya Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Iringa (Tumaini), Elius William, alisema wataendelea kutoa elimu kwa wanafunzi wa chuo hicho juu ya madhara yanayotokana na biashara ya ngono ambayo baadhi ya wanafunzi wanakuwa wanaifanya.

William aliwataka wanafunzi wa chuo hicho kuyaishi maisha ya chuo kwa kuangalia kilicho wapeleka kufika chuoni ili wafikie malengo yao na kusema kuwa starehe zipo tu haziishi duniani, hivyo watimize kwanza malengo ndio wafanye mambo mengine.

Naye Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Iringa, Prof. Ndelilio Urio, alimshukuru Mkuu wa Wilaya kwa kuwafunda wanafunzi hao kwa masuala mbalimbali ikiwamo madhara ya biashara ya ngono.



Mwanafunzi Jamila Issa wa kidato cha pili Shule ya Sekondari Makumbusho Dar es Salaam, akichangia mada juzi, katika mkutano wa kuwajengea uwezo wadau wa mapambano dhidi ya rushwa ya ngono kwa wanafunzi, mkutano huo uliandaliwa na Shirika la Wanawake katika Jitihada za Kimaendeleo (WAJIKI). **PICHA: SABATO KASIKA**

# 'Tusiwekeze kwenye elimu ya darasani pekee'

**Na Yasmine Protas**

IMEELEZWA kuwa mbinu za kufanikiwa kimaisha ni kuwekeza katika kujisomea vitabu mbalimbali vya ujasiriamali na si kuwekeza katika elimu ya darasani pekee.

Hayo yalisemwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Uongozi na Ujasiriamali (IMED), Dk. Dornald Olom, wakati wa uzinduzi wa kitabu kiitwacho 'Anza Kuwa na Staw'.

Dk. Olom alikuwa mgeni rasmi katika uzinduzi wa kitabu hicho kilichoandikwa na Prosper Lemmy Magali, ambaye ni Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wadau wa Nishati Jadidifu Tanzania( TAREA), pia ni mkurugenzi wa ubunifu na uendelezaji mradi wa Ensol (T) Ltd.

Dk. Olomi ambaye yupo katika kamati ya taifa katika maendeleo ya elimu nchini, alisema kazi ya kuboreshwa mitaala bado inafanywa ambapo mwaka 2015 mitaala katika topic zimeshawekewa kwa wanafunzi kuanzia darasa la tatu na kuendelea kusoma masuala ya ujasiriamali. "Changamoto ipo katika suala la elimu ambapo wapo baadhi ya wanafunzi wanamaliza darasa la saba hawajui kusoma na kuandika," alisema. Aliongeza kuwa inatakiwa kuwe na shule za mfano ambazo wanafunzi watafanya kitu na kitaonekana. Akizungumzia masuala ya biashara, alisema mtu anaanza na mtaji mdogo na baadaye anafika mbali kibiashara.

Alisema kuwa mbinu za kujifunza kukuza ujasiriamali ni kujifunza kusoma vitabu mbalimbali vya ujasiriamali. "Nchi imepiga hatua baada ya kuwasaidia watu njia mbalimbali za ujasiriamali," alisema.

Aliongeza kuwa nafasi ya familia katika malezi inatakiwa vijana wajengewe uwezo katika masuala la ujasiriamali.

Akizungumzia mfumo wa kisera na sheria, alisema kuwa mfumo wa kisera na kisheria uwepo kwa ajili ya kusimamia biashara.

Alisema kwanza mtu anatakiwa awe na kumbukumbu katika biashara zake, awe mwelewa katika ulipaji wa kodi. Magali alisema kuwa kitabu hicho kikisomwa kitawasaidia watu mbalimbali kubadilika kimaisha.

Alisema takwimu zinaonyesha watu asilimia 70 ndio walioajiliwa katika sekta binafsi. Aliongeza kuwa watu wanamaliza vyuo, lakini hawana ajira rasmi. "Ili kupunguza tatizo la ajira ni lazima kuwasaidia waweze kukua," alisema.

Aliongeza kuwa inatakiwa kukuza vipaji vyao ili waweze kunufaika na fursa zilizoko.

# Zawadi za 'MastaBata-Kivyako Vyako' mil. 30/-

**Na Mwandishi Wetu**

WATEJA 100 wa Wiki ya Tatu ya Kampeni ya 'NMB MastaBata - Kivyako Vyako,' walipatikana jana na kutwaa jumla ya Sh. milioni 10, hivyo kufanya zawadi zilizotolewa hadi sasa kufikia Sh. milioni 30 kati ya zaidi ya Sh. milioni 200 zinazoshindaniwa.

NMB MastaBata ni kampeni ya wiki 10 inayoendeshwa na Benki ya NMB, ikilenga kuhamasisha wateja kufanya malipo na manunuzi kwa njia ya kadi za MasterCard, Masterpass QR, Vituo vya Mauzo (PoS) na mtandaoni, ambako zaidi ya wateja 1,080 watazawadiwa pesa taslimu.

Katika kampeni hiyo, ambayo huu ni msimu wake wa tatu, wateja 100 kila wiki huzawadiwa Sh. 100,000 kila mmoja, huku washindi 25 wa droo za mwisho wa mwezi wakijishindia kiasi hicho cha pesa, ambako 'Grande Finale' ikitarajia kutoa washindi 30 watakaojinyakulia Sh. milioni 3 kila mmoja.

Akizungumza kabla ya droo hiyo iliyofanyika jijini Dar es Salaam, Ofisa Mwandamizi wa Biashara ya Kadi wa NMB, Saidi Kiwanga, alisema kampeni hiyo imeonyesha ufanisi mkubwa katika kuelimisha wateja wao kuwa kadi ni zaidi ya kutolea pesa, badala yake ni njia salama na nafuu ya kufanya malipo ya manunuzi mbalimbali.

"Katika wiki mbili zilizopita, wateja 200 wamejishindia Sh. milioni 20 na leo tutapata washindi wengine 100, hivyo kufikisha watu 300 walionufaika na zawadi za Sh. milioni 30. Hakuna changamoto yoyote katika wiki tatu za kampeni hii, zaidi ya ufanisi na elimu pana kwa wateja wetu ya kutambua uwanda mpana unaopatikana kupitia kadi zao na PoS.

"Kiasi hiki cha Sh. milioni 30 ni kati ya zaidi ya Sh. milioni 200 zinazoshindaniwa kwa wiki 10, ambako kila wiki tunawazawadia washindi 100, droo za mwisho wa mwezi tutatoa zawadi kwa wateja 25 na katika fainali mwishoni mwa kampeni hii mwezi Machi, tutakuwa na washindi 30 ambao watajitwalia Sh. milioni 3 kila mmoja," alisema Kiwanga.

Ofisa Msimamizi kutoka Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania (GBT), Elibariki Sengasenga, aliwahakikishia wateja wa NMB kuwa kampeni hiyo inaendeshwa kwa kufuata taratibu zote zinazosimamia na bodi yake na kuwataka kuondoa shaka juu ya upatikanaji wa washindi wake.

"GBT ni waratibu na wasimamizi wakuu wa Michezo ya Kubahatisha Tanzania. Jukumu letu ni kuhakikisha sheria, kanuni na taratibu zinafuatwa. Tunawahakikishia wateja wa NMB kuwa kampeni hii inatoa washindi kihalali, wawe huru kufanya matumizi kwa kadi ambacho ndio kigezo kikuu cha kuingia katika droo na bahati zao zitaamua ushindi wao," alisisitiza Sengasenga.

Nipashe
Spotika



NYOTA 10 WANAOWEZA KUBADILISHA KLABU 2022 UK. 12



Messi

# NYOTA WATANO WALIOFUNGA HAT-TRICK NYINGI BILA PENALTI

**LONDON, England**

KUFUNGA mabao matatu, 'hat-trick' ni moja ya mambo ya kuvutia na kufurahisha zaidi katika mchezo wa soka. Mfungaji wa hat-trick anapewa mpira ili aende nao nyumbani kuhifadhi ikiwa ni sehemu ya kumbukumbu yake.

Kulingana na aina ya mabao yaliyofungwa ambayo yanatengeneza hat-trick, tunaweza kusema ni ya aina chache tofauti. Moja ni hat-trick ambayo mchezaji amefunga kwa kichwa na miguu yote miwili. Pia kuna kitu kinaitwa 'pure hat-trick' ambapo hakuna bao kati ya hayo matatu linalofungwa kwa penalti.

Tuangalie wachezaji watano waliofunga hat-trick nyingi bila penalti, twende sasa...

**#5. Sergio Aguero - hat-trick 10**

Maisha ya soka ya Sergio Aguero yalifikia kikomo kuelekea mwishoni mwa mwaka 2021. Mchezaji huyo wa zamani wa kimataifa wa Argentina, alilazimika kutundika daluga kutokana na tatizo la moyo. Aguero hakika alionekana kama alikuwa na mengi zaidi ya kutoa katika kiwango cha juu, lakini kutokana na hali yake ya kiafya, ilimbidi kutathmini upya vipaumbele vyake.

Aguero ataingia kwenye historia kama mmoja wa washambuliaji bora wa kizazi chake. Alitumia miaka yake kule Manchester City na ametengeneza jina lake kwenye Ligi Kuu England.

Aguero amefunga hat-trick 10 bila penalti katika maisha yake ya soka. Hicho ni kielelezo tosha cha jinsi mshambuliaji huyo alivyokuwa mahiri kiufundi na mwenye uwezo mzuri.

**#4. Robert Lewandowski - hat-trick 16**

Robert Lewandowski ndiye mshambuliaji mahiri zaidi katika ligi tano bora za Ulaya kwa sasa. Mshambuliaji huyo wa Bayern Munich amefunga angalau mabao 40 katika kila msimu kwa misimu sita kati ya 10 iliyopita. Lewandowski bila shaka ndiye mshambuliaji bora wa kizazi chake.

Tayari amefunga mabao 31 na kutoa asisti tatu katika mechi 26 kwenye michuano yote akiwa na Bayern Munich msimu huu. Katika msimu wa 2020-21, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33, alivunja rekodi ya muda mrefu ya Gerd Muller ya kufunga mabao mengi katika msimu mmoja wa Bundesliga (40) kwa kufumania nyavu mara 41.

Lewandowski amefunga hat-trick 16 bila penalti katika maisha yake ya soka.

**#3 Luis Suarez - hat-trick 21**

Luis Suarez ni mmoja wa washambuliaji bora wa karne ya 21. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Uruguay ana tofauti ya nadra ya kuwapita Lionel Messi na Cristiano Ronaldo katika ubora wao.

Alifanya hivyo msimu wa 2015-16. Suarez alifunga mabao 40 katika mechi 35 za La Liga msimu huo. Aliunda umoja wa washambuliaji watatu bora zaidi kule Barcelona akiwa na Lionel Messi na Neymar Jr.

Suarez ni mmoja wa washambuliaji kamili wa wakati wote. Ana kasi, nguvu, uwezo mkubwa wa kupiga chenga na pia ana akili sana katika ukimbiaji wake. Mchezaji huyo wa Uruguay pia ni bora katika uchezaji wa kiungo jambo ambalo lilimfanya kuwa fiti kabisa akiwa Barcelona wakati wa miaka yake pale.

Suarez amefunga hat-trick 21 bila penalti katika maisha yake ya soka.

**#2. Cristiano Ronaldo - hat-trick 27**

Cristiano Ronaldo ndiye mchezaji aliyefunga hat-trick nyingi zaidi katika historia ya mchezo huo. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno ni mmoja wa wanasoka bora zaidi wa wakati wote na kwa urahisi ni mmoja wa wafungaji bora kuwahi kupamba mchezo huo.

Ronaldo amefunga hat-trick 58 katika maisha yake ya soka. Mshambuliaji huyo amekuwa mfungaji wa penalti mkuu kwa klabu na nchi kwa sehemu kubwa ya maisha yake.

Ronaldo amefunga mabao mengi kwa mikwaju ya penalti. Ukiondoa penalti, Ronaldo ana hat-trick 27.

**#1. Lionel Messi - 41 hat-trick**

Lionel Messi hivi karibuni alitwaa Ballon d'Or ya saba na kuweka rekodi ya aina yake. Bila shaka ndiye mwanasoka bora zaidi wa wakati wote. Hatujaona mchezaji yeyote mwenye ustadi wa asili wa mchezo kama Messi.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Argentina ni mzuri sana akiwa na mpira miguuni mwake, akiwapita mabeki kwa urahisi na kufunga mabao ya ajabu kutoka popote anapopenda.

Alifunga mabao 91 mwaka 2012 ambayo ni idadi kubwa ya mabao kuwahi kufungwa katika kipindi cha mwaka mmoja wa kalenda. Messi ana hat-trick 55 katika maisha yake ya soka. 41 kati ya hizo amefunga bila penalti na inaonyesha ni jinsi gani mshambuliaji huyo ni hatari.

## ISIKUPITE

MSHAMBULIAJI wa Manchester United, Cristiano Ronaldo, ndiye mchezaji aliyefunga mabao mengi zaidi kwa kichwa (110), kuliko mchezaji yeyote yule katika karne hii ya 21, akifuatiwa na Luuk de Jong (Barcelona) mabao 77 na Robert Lewandowski (Bayern Munich) mabao 77.



## Extra Time



Mbappe

# NYOTA 10 WANAOWEZA KUBADILISHA KLABU 2022

**LONDON, England**

SIO kila mchezaji wa soka amejengwa sawa, na ni wale bora tu ndio wanaoweza kutawala uwanja na kubaki kukumbukwa na mashabiki kwa muda mrefu. Lakini soka si tu sifa za kimichezo, kwani soka la klabu za sasa pia limekuwa biashara kubwa. Kwa hivyo haijalishi mchezaji wa soka ni mkubwa kiasi gani katika klabu fulani, kutafuta ukuaji, changamoto mpya au malipo bora kunaweza kuwafanya wabadilike.

Miaka miwili iliyopita imeshuhudiwa wachezaji wengi wakibadilisha klabu licha ya dhiki ya kifedha kutokana na mlipuko wa ugonjwa wa Covid-19. Lionel Messi na Cristiano Ronaldo walihama msimu uliopita, wakijiunga na Paris Saint-Germain na Manchester United.

Mwaka huu vile vile, kuna nyota kadhaa ambao wanaweza kubadilisha klabu. Katika makala haya tunawachambua, twende sasa...

### #10. Harry Kane

Majira ya joto ya mwaka 2021, yalishuhudia tetesi nzito za Harry Kane kutaka kuhama kutoka Tottenham Hotspur kwenda Manchester City. Ingawa nahodha huyo wa England aliomba msamaha baadaye, mambo yaligeuka kuwa mabaya pale Kane aliporipotiwa kukosa mazoezi katika mechi za kujiandaa na msimu mpya.

Mwisho, Kane aliamua kubaki Tottenham huku Manchester City wakielekeza mawazo yao kwingine. Hii ilitokana hasa na upinzani wa Daniel Levy kwa aina yoyote ya uhamisho, bila kujali fedha zinazohusika.

Msimu wa sasa kwa Kane umekuwa mbaya zaidi katika rangi za Tottenham. Mabao yake 12 katika mechi 28 yanaweza kuonekana kuwa sawa, lakini ameweza kufunga mabao manne pekee katika mechi 17 alizocheza kwenye Ligi Kuu England.

Kane amebakiza miaka miwili zaidi kwenye mkataba wake. Lakini inaonekana kuna uwezekano zaidi Tottenham wanaweza kumuuza kwa klabu itakayofikia bei yake.

### #9. Antonio Rudiger

Tangu Thomas Tuchel aanze kuinoa Chelsea mwaka 2021, Antonio Rudiger amekuwa mmoja wa wachezaji muhimu zaidi wa kikosi hicho. Akicheza kama sehemu ya walinzi watatu wa kati.

Rudiger alitoa mchango kwa 'The Blues' hao wakati wakibeba taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka jana.

Rudiger alipoingia mwaka wa mwisho wa mkataba wake msimu wa majira ya joto wa 2021, mashabiki wengi wa Chelsea walitarajia kupata suluhisho la haraka. Hata hivyo, haikuwa hivyo kwani Rudiger na Chelsea hawajaweza kufikia makubaliano kuhusu mshahara wake.

Mazungumzo bado yanaendelea, lakini kumekuwa na nia kutoka kwa klabu nyingine. Masuala hayo yasipotatuliwa haraka, huu utakuwa msimu wa mwisho kwa Rudiger ndani ya Chelsea.

### #8. Jude Bellingham

Jude Bellingham alipoingia katika kikosi cha kwanza cha Birmingham City, alikuwa ameingia kwenye ujana wake.

Manchester United walihusishwa na kuwania saini yake. Lakini kiungo huyo wa kati wa England alikuwa akitafuta dakika za uhakika jambo ambalo lilimfanya aende Borussia Dortmund. Nchini Ujerumani, amepanda daraja haraka na kuwa mmoja wapo wa vijana wenye vipaji vya hali ya juu zaidi duniani.

Ingawa bado ana muda uliosalia kwenye mkataba wake, Bellingham amekamata vichwa kadhaa vya habari katika mwaka uliopita. Amekuwa imara msimu huu kwa kutoa asisti 10 na mabao manne katika mechi 26 alizocheza.

Lakini wababe wengi wa Ulaya hawana uhaba wa fedha hivyo Bellingham anaweza kuondoka.

### #7. Franck Kessie

Franck Kessie amekuwa mmoja wa viungo wa kati bora zaidi katika siku za hivi karibuni. Raia huyo wa Ivory Coast amejizolea umaarufu mkubwa akiwa na AC Milan, na klabu kadhaa zimekuwa zikimfuatilia.

Klabu hizo pia zimezingatia kumalizika kwa mkataba wake. Licha ya mazungumzo kadhaa mwaka jana, bado hakuna suluhu.

Kuna uwezekano mkubwa kwa Kessie kuondoka pale Milan mwaka huu.

Hata hivyo, Kessie amefunga mabao matano na asisti moja katika mechi 21 alizocheza hadi sasa.

### #6. Declan Rice

Declan Rice ni mmoja wa wachezaji wa kati vijana bora kwenye Ligi Kuu England. Baada ya kuonyesha kiwango kizuri kwenye michuano ya Euro, klabu nyingi zimekuwa zikimkodolea macho.

Ripoti zilimhusisha na kurejea katika klabu yake ya utotoni, Chelsea, huku pia akihusishwa na kuhamia Old Trafford. Mahitaji ya West Ham yalikuwa makubwa sana na ilisaidia klabu hiyo ya London kuendelea kumshikilia mchezaji wao hadi sasa.

Amekuwa mmoja wa wachezaji nyota wa West Ham msimu huu na kuwafanya 'Wagonga Nyundo' hao kufanya zaidi ya ilivyotarajiwa. Kwa sasa wako katika nafasi ya nne kwenye msimamo wa ligi na wako pia katika hatua ya mtoano ya Ligi ya Europa.

Zaidi ya hayo, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, atakuwa na miaka miwili iliyosalia kwenye mkataba wake na tayari ameonyesha nia yake ya kuhama.

### #5. Luis Suarez

Kosa kubwa la kocha wa zamani wa Barcelona, Ronald Koeman linaweza kuwa ni kutomthamini mshambuliaji wa Uruguay, Luis Suarez. Suarez al-

ionekana kutohitajika na aliuzwa kwa Atletico Madrid mwaka 2020.

Suarez alifanikiwa kutwaa taji la Ligi Kuu Hispania akiwa na Atletico katika msimu wake wa kwanza na alikuwa mmoja wa wachezaji bora kwenye ligi.

Licha ya kuwa na umri wa miaka 34, Suarez ameonekana mkali msimu huu. Kasi yake inaweza kuwa imepungua, lakini umaliziaji wake unabaki kuwa mzuri.

Tayari amecheza mechi 27 na amefunga mabao tisa na kutengeneza pasi mbili za mabao. Huku mkataba wake ukikamilika msimu wa majira ya joto unaokuja na anaweza kuwa katika klabu mpya.

### #4. Paul Pogba

Msimu wa pili wa msukosuko kwa Mfaransa huyo huko Manchester United unaonekana kumalizika. Paul Pogba alinunuliwa kwa ada kubwa ya uhamisho (pauni milioni 75) kutoka Juventus na wakati fulani alikuwa mchezaji wa kiwango cha dunia.

Lakini kukaa kwake Old Trafford kumekumbwa na majeraha na utata. Pogba mara nyingi amekuwa akipata shida kutokana na wakala wake kuweka wazi kuwa anatakiwa na klabu nyingine ikiwamo Manchester City.

Msimu wa Pogba wa 2021-22 ulianza vema dhidi ya Leeds United, ambapo alikuwa na hat-trick ya asisti.

Manchester United wameripotiwa kuweka mezani mkataba mpya, lakini uwezekano ni kwamba Pogba anaweza kuondoka kwenda kwenye malisho mapya.

### #3. Dusan Vlahovic

Dusan Vlahovic bila shaka anaweza kutwaa nafasi ya juu kati ya nyota kadhaa wanaokuja juu kwenye Serie A. Kama Kane, Vlahovic pia alipendekezwa kuhamia Manchester City kwa sehemu kubwa ya dirisha la usajili la majira ya joto lililopita.

Hivi majuzi, amekuwa akipigiwa upatu kuhamia Arsenal, ambako kuna uwezekano mkubwa atachukua nafasi ya Pierre-Emerick Aubameyang. Sababu pekee iliyofanya hatua za Vlahovic kutotimia ilikuwa ni matakwa kupita kiasi ya Fiorentina. Hata hivyo, Vlahovic atakuwa amebakiwa na mwaka mmoja pekee katika mkataba wake mwaka huu. Hivyo, Fiorentina watatafuta fedha nyingi kadiri wawezavyo kwa ajili yake.

Amekuwa katika kiwango cha juu msimu wa sasa, ambapo Vlahovic ameonyesha ulimwengu kikamilifu uwezo wake. Amecheza mechi 23 katika michuano yote mikubwa, ambapo Mserbia huyo amefunga mabao 19 na kutengeneza mengine matatu.

Hata hivyo, kutokana na klabu kadhaa kutafuta mshambuliaji mpya katika dirisha la majira ya joto, Vlahovic anaweza kujikuta katika jezi mpya.

### #2. Erling Haaland

Moja ya uhamisho mkubwa ambao haukufanyika msimu uliopita wa majira ya joto ungekuwa ni mabadiliko ya Erling Haaland kwenda Chelsea. Klabu hiyo yenye maskani yake London ilimtaka mwanasoka huyo wa Norway msimu mzima, lakini haikuwa hivyo. Waliishia kumsajili Romelu Lukaku kutoka Inter Milan.

Lakini hiyo haimaanishi kwamba Haaland hataweza kuhama msimu huu. Kulingana na walioidhinishwa hivi majuzi na mchezaji, hata kuhama katika dirisha hili la majira ya baridi bado hakuwezi kutengwa. Haaland anaripotiwa kuwa ana kifungu cha kutolewa cha karibu euro milioni 80 ambacho kitaanza kutumika katika dirisha lijalo la majira ya joto.

Kwa bahati mbaya, Haaland alivumilia jeraha msimu huu, lakini hilo halijaathiri uwezo wake wa kufunga mabao. Katika mechi 18 alizocheza, amefunga mabao 21 na kusaidia mengine sita.

### #1. Kylian Mbappe

Ikiwa Kylian Mbappe atahama majira ya joto, unaweza kuwa usajili mkubwa zaidi wa mchezaji huru. Nyota huyo amekuwa mshindi tangu alipotoka kule Monaco akiwa katika umri mdogo. Ameendelea kuwa na nguvu na ameshinda Kombe la Dunia akiwa na Ufaransa mwaka 2018.

Mbappe anaweza kucheza katika nafasi yoyote kwenye safu ya ushambuliaji kwa ustadi mkubwa. Anatumia kasi na ujuzi wake.

Mbappe amebakiza chini ya miezi sita katika mkataba wake wa sasa na PSG. Amekuwa akihusishwa na Real Madrid kwa muda mrefu, lakini klabu nyingine pia zinaripotiwa kuwa kwenye kinyang'anyiro hicho.

Bado haijafahamika iwapo Mbappe ataongeza mkataba wake au la. Mbappe tayari ameichezea klabu hiyo ya Paris mara 27 msimu huu. Katika mechi hizo, Mfaransa huyo amefunga mabao 19 na kusaidia kutengeneza mabao 15.

## Nukuu

"Ushindi mmoja muhimu zaidi kabla ya Ligi Kuu England kusimamishwa, hatua moja zaidi kuelekea malengo yetu. Njia ni ngumu na imejaa vikwazo, lakini tunasimama pamoja na kufanya kazi kwa bidii ili kuwafanya mashabiki wetu wajivunie! Twendeni, Mashetani!," **Mshambuliaji wa Manchester United, Cristiano Ronaldo akielezea furaha yake baada ya ushindi wa bao 1-0 dhidi ya West Ham juzi.**



"Jota hayupo mbali kufikia alichofanya Mo Salah Liverpool. Salah alipoletwa, macho yote yalielekezwa mchezoni. Ndivyo hivyo hivyo kama ilivyo kwa Jota," **Nyota wa zamani wa Ireland, mshambuliaji Tony Cascarino akisifu usajili unaofanywa na Kocha wa Liverpool, Jurgen Klopp.**



"Unapokuwa Kocha wa Chelsea, hauko katika eneo salama. Kila mmoja anatarajia mengi - mmiliki na bodi pia. Kuna kiwango na unakubali. Unapopewa kazi, unakubali," **Nyota wa zamani wa Chelsea, Florent Malouda akitoa maoni yake kuhusu nafasi ya Kocha Thomas Tuchel hapo darajani.**



Nipashe Spotika

NIPASHE JUMATATU JANUARI 24, 2022

# WACHEZAJI WA4 SIMBA WALIVYOIBEBA MTIBWA




Kiungo mshambuliaji wa Simba, Pape Sakho, akijaribu kumtoka beki wa Mtibwa Sugar, Hassan Banda (aliyepiga magoti), lakini mabeki wengine Ibrahim Ame, karibu yake wakiweka ulinzi mkali na Salum Kanoni (kushoto), wakati timu hizo zikitoka suluhu juzi. **MPIGAPICHA WETU**

**a Adam Fungamwango**

NI mechi iliyochezwa Uwanja wa Manungu Complex, Turiani, mkoani Morogoro juzi jioni kwa mara ya kwanza baada ya miaka 23, kati ya wenyeji Mtibwa Sugar dhidi ya mabingwa watetezi, Simba.

Iliisha kwa sare ya bila kufungana, ikiwa ni moja ya mechi ya Ligi Kuu Tanzania, ikichezwa kwenye hali ya uwanja kutuama maji baadhi ya maeneo na matope pia kiasi cha wachezaji wa pande zote mbili kutumia mifumo ya wachezaji wao, lakini kujiongeza wenyewe kwa sababu kuna wakati uwanja ulikuwa hauruhusu.

Mtibwa Sugar ilionekana kuisoma zaidi Simba kuliko wageni kuwasoma wenyeji. Licha ya Kocha Mkuu Salum Mayanga kujua mara nyingi timu ya Simba inacheza mfumo gani na kwenye uwanja kama ule jinsi ulivyo watacheza vipi, lakini kwa kiasi kikubwa wachezaji wa Mtibwa Sugar walionekana kuifahamu vizuri Simba, hivyo kuziba mianya yote ambayo waliona wataitumia.

Na hii ilichagizwa na kuwapo kwa wachezaji watano ambao wamewahi kuicheza Simba.

Katika makala haya tunawaangalia wachezaji hao wa Mtibwa Sugar ambao wamewahi kuichezea Simba kwa vipindi tofauti na wengine wakiwa huko kwa mkopo.

**#1. Salum Kanoni**

Alicheza namba mbili kwenye mechi ya juzi na alikuwa msaada mkubwa kwa timu yake ya Mtibwa Sugar na kuwapa wakati mgumu wachezaji wa Simba, hasa Gadiel Michael ambaye alikuwa anashindwa kupanda, lakini hata mara chache alizofanikiwa, hakuweza kupiga krosi kwa usahihi.

Alimsaidia Salum Kihimbwa kumtesa Gadiel, na mara nyingi Mtibwa Sugar walionekana kushambulia upande huo.

Kanoni alikuwa mchezaji wa Simba kuanzia 2010 hadi 2012 na kuichezea timu hiyo kwa mafanikio makubwa hadi 2010, alipoondoka na kwenda kujiunga na Kagera Sugar kuchukua nafasi ya Ally Shomari ambaye yeye alijiunga na Simba. Mwaka 2017, Kanoni alisajiliwa na Mtibwa, timu ambayo anaichezea hadi leo.

**#2. Hassan Banda**

Ni beki wa kati ambaye naye alicheza mechi ya juzi na kuwa kikwazo kikubwa kwa mastraika wa Simba kama Meddie Kagere, Chriss Mugalu na hata John Bocco alipoingia.

Alihakikisha hawaleti madhara, ingawa kuna wakati alikuwa akicheza rafu zisizo na msingi, kiasi na alikuwa na bahati tu ya kutotolewa kwa kadi nyekundu kutokana na aina ya mchezo wake usiokuwa wa kiungwana.

Nadhani alifahamu kuwa wachezaji wengi wa Simba kuwa hawapendi kugongana na ukifanya hivyo wanakuwa waoga. Aliichezea Simba mwaka 2014 akitokea Coastal Union, na kuhudumu kwa miaka mitatu hadi 2017, alipotimkia Baroka FC ya Afrika Kusini.

**#3. Ibrahim Ame**

Huyu bado ni mchezaji wa Simba, anayeichezea Mtibwa Sugar kwa mkopo. Mkataba wake utaisha Juni 30, 2023. Alipelekwa kwenye klabu hiyo mwanzoni mwa msimu huu. Ni beki wa kati aliyetengeneza upacha na Banda na kwa kiasi kikubwa waliweza kuwamudu mastraika wa Simba.

Anawafahamu vilivyo wachezaji wa timu yake mama na jinsi ya kuwakabili, hivyo haikuwa tabu kwake. Alijiunga na Simba Agosti 25, 2020, akitokea Coastal Union, lakini kutokana na ushindani wa namba, akapelekwa Mtibwa Sugar kwa mkopo.

**#4. Said Ndemla**

Ni mchezaji ambaye ni zao la kikosi cha pili cha Simba, na alipandishwa rasmi kucheza timu ya wakubwa 2013 na amedumu kwa miaka yote, hadi mwaka jana Septemba 4, alipotolewa kwa mkopo Mtibwa Sugar.

Naye alicheza kwenye mechi ya juzi, akionyesha kiwango cha hali ya juu na kujituma, tofauti na alivyokuwa Simba. Alionekana kugongana na wachezaji wa timu yake ya zamani, tofauti na alivyokuwa akicheza timu yake hiyo. Nusura afunge bao, baada ya kuchia kombora kali la mbali kama kawaida yake, lakini ukapita juu, na pia aligongana na Manula, katika harakati za kutaka kuukwamisha mpira wavuni.

**JE, WAJUA?**



Katika michezo 12 ya awali msimu uliopita, Klabu ya Simba ilikuwa imevuna pointi 26 kama ilivyo hadi sasa msimu huu ambapo imejikusanyia alama 26 kutoka mechi 12, lakini pia wakati huo Yanga ndiyo iliyokuwa ikiongoza msimamo wa ligi kama ilivyo sasa.





Mtetezi wa Haki wa Jumuiya ya Kikristo Tanzania (CCT), Mchungaji John Kamoyo (kushoto), akitoa mada katika mafunzo kwa waandishi wa habari Mkoa wa Dodoma yaliyofanyika mwisho wa wiki, kuhusu kuandika habari za utetezi katika makundi mbalimbali katika jamii. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Jenerali Mabeyo ataka JWTZ kubuni miradi kimkakati

**Na Paul Mabeja**, DODOMA

MKUU wa Majeshi Nchini, Jenerali Venance Mabeyo, amevitaka vikosi vya Jeshi la Wananchi (JWTZ) kutumia wataalamu wa ndani kubuni miradi ya kimkakati na kuhimiza uadilifu kwenye miradi iliyokamilika.

Jenerali Mabeyo, aliyasema hayo juzi wakati akizindua kituo cha mafuta cha kikosi cha Jeshi cha R 971 kilichoko Ihumwa, jijini Dodoma.

Alisema jeshi kama taasisi linaweza kufanya mambo makubwa, kinachotakiwa ni kujiamini, kuwa na mitazamo chanya wakati wote na wabunifu katika miradi hiyo.

"Hakuna kisichowezekana wenzetu wameweza kwanini sisi tusiweze, kuna taaluma nyingi ndani ya jeshi, lakini tumezilaza, tuziibue taaluma tulizonazo kwa manufaa ya jeshi na taifa kwa ujumla, mimi bado naamini inawezekana," alisema.

Alisema pamoja na kuwa serikali ina wajibu wa kulihudumia jeshi kwa asilimia 100, bado kuna haja ya jeshi kuwa na mchango kwa nchi kama ilivyo kwa majeshi mengine duniani kwa kuanzisha miradi mbalimbali.

"Nilipata fursa za kutembelea maeneo ya ndani na nje ya nchi yakiwamo majeshi makubwa, wenzetu huko wanafanya mambo makubwa na wanachangia uchumi na pato la taifa, lakini sisi tulikuwa tunategemea serikali kwa asilimia 100. Wajibu wa serikali kulihudumia jeshi ni kweli, ndiyo dhana, je, sisi hatuna mchango wowote? Mchango wetu ni kuhakikisha tunachochea ukuaji uchumi na jukumu letu la msingi la ulinzi wa nchi na haya yanawezekana," alisisitiza.

"Tuliona tusiwe walalamikaji tutumie fursa kulingana na mazingira yetu huku tukiwatumia askari wachache na wengine wakiendelea na jukumu la msingi na tulianza na miradi midogo midogo, lakini tumeanza vizuri," aliongeza.

Mabeyo alisisitiza vikosi kuendelea kuimarisha miradi iliyokwisha kamilika na kufikiria mikubwa zaidi na ya kimkakati.

"Fikra hizo ni lazima tuelekeze kwenye ubunifu, tubuni miradi mikubwa na ya kimkakati kama huu (kituo cha mafuta). Watu hawaelewi kama mafuta ni mradi wa kimkakati, mafuta yakikosekana katika nchi ina paralyze nchi na ikiparalyze hakuna usalama ndiyo maana nilifikiria hili lazima tulibebe maana ni suala la kimkakati na la kiusalama," alisema.

Mabeyo alisema kwa sasa jeshi linaangalia uwezekano wa kuagiza mafuta moja kwa moja ili kuwa na akiba ya nchi na mitambo ya kusafisha mafuta.

"Tumeanza mchakato wa kuhakikisha tunaagiza mafuta moja kwa moja kutoka kwa wenye visima na tayari timu yetu iko nje kufanya mazungumzo. Ninaamini tukifanya hivyo tutakuwa na mkakati wa kuhifadhi mafuta kwa usalama wa nchi, lakini kitakuwa chanzo cha mapato ya kusaidia kusonga mbele," alisema.

"Ifike mahala tuanzishe mitambo ya kusafisha mafuta ghafi, tukifanya hivyo tutapata bidhaa nyingi sana kama vile mafuta ya ndege, ya taa, lami na kuweka mkakati wa kuhifadhi mafuta kila mahali," alisisitiza.

Alisema kikosi cha R 971 ni miongoni mwa vikosi vitatu vikiwamo vya 12 KJ na 27 KJ ambavyo vimeanzisha miradi ya kimkakati na kuahidi kukipatia kituo hicho Sh. milioni 100 kwa ajili ya kukipa uwezo zaidi.

Alilipongeza Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) kwa kuwa mfano wa kutekeleza miradi ya kimkakati ukiwamo wa skimu ya umwagiliaji ambao umelenga kujilisha na kuweka akiba ya chakula.

"Wenzetu wa Jeshi la Kujenga Taifa wameshaanzisha miradi ya kimkakati ambayo inalenga kujilisha na kuwa na akiba ya chakula itakayolipatia taifa usalama wa chakula, nchi ikikosa chakula inakuwa na njaa na kukiwa na njaa kunakuwa hakuna amani, hakuna utulivu JKT wana uwezo wa kufanya hivyo," alisema.

Awali, Kamanda wa Kikosi cha R971 Ihumwa, Kanali Justus Kitta, alisema kituo hicho kimejengwa kwa gharama ya Sh. milioni 280 kikiwa na matangi yenye uwezo wa kuhifadhia lita 60 za mafuta.

Alisema mkakati ulioko ni kuongeza visima zaidi na kujenga kituo kingine jijini Dodoma kabla ya kuwa na vituo vya mafuta kila mkoa.

## Bashungwa ataka taarifa ujenzi madarasa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Inoccent Bashungwa, amewaagiza wakuu wa mikoa taarifa za ujenzi wa vyumba vya madarasa 15,000 zinawasilishwa kabla ya Januari 25 ili vianze kutumika na wanafunzi.

Aidha, ameitaka Tume ya Utumishi wa walimu kuunda dawati la kusaidia wastaafu kudai mafao ya uzee ili wasisumbuliwe.

Bashungwa aliyasema hayo wakati wa ufunguzi wa Baraza la Wafanyakazi wa Tume hiyo liliofanyika jana jijini hapa.

Alisema taarifa ya ujenzi wa vyumba hivyo ambavyo vimegharamiwa na fedha za serikali inapaswa kuwasilishwa mapema kabla ya tarehe hiyo, ili vianze kutumika kama walivyokubaliana tangu ujenzi huo unaanza.

"Naomba wakuu wa mikoa muende mkajiridhishe kwa sababu nahitaji taarifa iliyosahihi ndani ya tarehe niliyoitaja au kabla ya tarehe hiyo," alisema Bashungwa.

Alisema anahitaji kuona vyumba hivyo vinakamalika kwa wakati lengo ni kuona wanafunzi hawapati shida wakati wa masomo yanapoendelea.

Aliitaka tume hiyo kuanzisha dawati la kusaidia wazee wastaafu kudai mafao yao ili wasiteseke kutokana na kazi waliyofanya wakiwa katika utumishi wao wa umma.

Alisema wanapaswa kuanzisha dawati hilo ambalo litakuwa mstari wa mbele kupokea malalamiko ya wastaafu wanapokuwa wanadai mafao yao ili waweze kuwasaidia kuyapata haraka.

Bashungwa alisema anasikitishwa na vitendo vya utoro kwa walimu jambo ambalo linachangia kurudisha taalumu yao nyuma.

Alisema walimu wanapaswa kuchukuliwa hatua kali dhidi ya makosa hayo ili iwe fundisho kwa wengine ambao wanafanya makosa kama hayo wakiwa kazini.

"Hiki kitendo sio kizuri kabisa kwa walimu kwa sababu kinadhalilisha taaluma, mwalimu ni kioo cha jamii kwanini alete uzembe," alisema Bashungwa.

# Wakulima zabibu kuwezeshwa kujenga viwanda

**Na Paul Mabeja**, DODOMA

WAZIRI wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji, amesema serikali ipo tayari kuwawezesha wakulima wa zabibu mkoani Dodoma kujenga viwanda ili kuongeza mnyororo wa thamani wa zao hilo.

Dk. Ashatu alibainisha hayo juzi jijini hapa katika ziara ya kukagua maeneo ya uwekezaji ya mamlaka ya maeneo maalumu ya uzalishaji kwa mauzo ya nje (EPZA) katika eneo la Nala.

Alisema Mkoa wa Dodoma ni eneo la kimkakati na zabibu inayozalishwa haizalishwi sehemu nyingine duniani.

"Hatuna viwanda ikifika muda wa kuvuna Mkuu wa Mkoa unaanza kushika tumbo, nawakaribisha wawekezaji waje wawekeze Mkoa wa Dodoma ni miongoni mwa mikoa mitatu ya kimkakati sasa tukisha zalisha zabibu zetu tunazipeleka wapi? Sisi tupo tayari kushirikiana na sekta binafsi ili tuweze kuwakwamua wakulima wetu.

"Tukiacha zabibu tuna zao la alizeti, Dodoma pia alizeti ipo kwenye zao la kimkakati tuone namna gani tunaweza kujikwamua na zao hili hata reli yetu ya kisasa inapokamilika sisi tuwapelekee mafuta," alisema.

Mkurugenzi Mkuu wa EPZA, Charles Itembe, alisema tangu kuanzishwa kwake, imetoa leseni kwa kampuni 18.

Alisema kampuni hizo zimewekeza mtaji wa jumla ya Dola za Kimarekani bilioni 2.549, mauzo nje Dola za Kimarekani bilioni 2.497 na kutoa ajira za moja kwa moja kwa watu 64,159 kufikia mwezi Desemba, 2021.

Alisema jitihada za Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma na Ofisi ya Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma kwa kufanikisha ubainishaji na kulitenga eneo hilo kwa matumizi ya kuwa eneo maalum la uwekezaji.

"Mamlaka ya EPZ kwa mujibu wa majukumu yake kisheria, tutaliendeleza eneo hili kama kitivo maalum cha Ugavi, Biashara na Viwanda - (Trade, logistics and industrial park), kwa kuzingatia nafasi ya kijiographia ya Mkoa wa Dodoma kwa kuvutia mitaji ya uwekezaji katika sekta ya kilimo (kuongeza thamani ya mazao yanayozalishwa katika mikoa ya kanda ya kati kama vile alizeti, zabibu, karanga na mifugo)," alisema.

Sekta nyingine zinazotegemewa kuvutia uwekezaji katika eneo la mradi ni pamoja na ujenzi, madini, dawa na mavazi.

"Serikali ilianzisha Mamlaka ya Maeneo Maalumu ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje, mwezi Februari, 2006. Uamuzi huo, ulitekelezwa kupitia marekebisho ya sheria namba 11 ya mwaka 2002 yaliyopitishwa na Bunge ili kusimamia utekelezaji wa programu ya Export Processing Zone (EPZ)," alisema.



# Asilimia 27 waripoti kidato cha kwanza wilayani Mbarali

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

ASILIMIA 27 ya wanafunzi waliofaulu kujiunga na kidato cha kwanza kati ya 6,200 wilayani Mbarali ndio pekee hadi sasa wameripoti kuanza masomo.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, Missana Kwangura, hadi kufikia Ijumaa ya wiki iliyopita ni asilimia 27 ya wanafunzi waliofaulu kujiunga na kidato cha kwanza waliripoti shule.

Kutokana na mwitikio wa wanafunzi kuripoti shule, Kwangura alitumia mwanya huo kuwahamasisha wazazi na walezi kupeleka watoto shule.

Alisema hata kama bado hawajashonewa sare waanze ili kuendelea na masomo kuliko kubaki nyumbani, na kwamba wataendelea kutembea nyumba kwa nyumba kuhimiza watoto kuripoti shuleni ili kupata haki yao ya msingi kwa sababu serikali imejenga miundombinu yote ya shule. "Tunahimiza wazazi na walezi kuwapeleka watoto shule kuanza masomo hata kama hawana sare za shule, mwitikio bado hauridhishi ni asilimia ndogo ya walioripoti vyumba vya madarasa, madawati na miundombinu mingine imekamilika hakuna upungufu," alisema Kwangura.

Aliongeza kuwa uandikishaji wa wanafunzi wa awali na darasa la kwanza hadi sasa umefikia asilimia 30 tu, hivyo wanaendelea kuhamasisha wazazi kuwaandikisha watoto ambao wamefikia umri wa kuanza masomo.

Alisema vilevile vituo shikizi vinaendelea kupokea wanafunzi wa awali, lengo ni kuwapunguzia adha watoto kutumia umbali mrefu kwenda shule na kuwaepusha na athari kama vile za wanyama njiani.

Mwalimu Mkuu Shule ya Msingi, Manienge, Bryson Lutambi, ambaye anahudumia kituo shikizi cha Mabambila, alisema walipokea shilingi milioni 80 kwa ajili ya kujenga vyumba vinne vya madarasa.

Alisema kituo hicho kitawapunguzia adha watoto kutembea umbali wa kilomita sita kwenda shule mama ya Manienga, na kwamba fedha za ujenzi walizipokea kutoka Luhanga.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, Twalibu Lubandamano, alisema ujenzi wa kituo hicho unatokana na fedha zilizoelekezwa kujenga shule katika Kata ya Luhanga ambazo zinatokana na GN namba 28 waliamua kuzihamisha kwenda maeneo mengine.



Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, Twalib Lubandamo (katikati), juzi akitoa ufafanuzi kwa wanahabari (hawapo pichani) kuhusu matumizi ya fedha Sh. milioni 160 zilizotolewa na serikali kwa ajili ya kujenga vituo shikizi Kata ya Luhanga, ambazo hivi karibuni ziliripotiwa hazijulikani ziliko fedha hizo, wapili kulia ni Mkuu wa Wilaya ya Mbarali Reuben Mfune.
**PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Afa kwa kusombwa na mafuriko akitokea kilabuni

**Na Grace Mwakalinga,** SONGWE

MKAZI wa Kitongoji cha Mlambwizi katika Kijiji cha Chimbuya wilayani Mbozi mkoani Songwe, Sipendeki Mdollo (34), amekutwa amekufa kutokana na kusombwa na maji ya mvua wakati akirudi nyumbani kwake akitoke kwenye kilabu cha pombe.

Kwa mujibu wa Mwenyekiti wa Kitongoji hicho, Hestin Mnkondya, tukio hilo lilitokea Januari 19, mwaka huu, kati ya saa mbili usiku wakati Mdollo akirudi nyumbani kwake.

Mnkondya alisema wakati Mdollo akirejea nyumbani alikuta mto umefurika kufuatia mvua zinazoendelea kunyesha, na kwamba inasadikiwa aliteleza na kutumbukia katika mto huo na kusombwa na maji.

"Mwili wa Mdollo ulikutwa Januari 20 karibu na bwawa la samaki linalomilikiwa na Givewelo Simbeye ambaye baada ya kukuta mwili huo eneo hilo nilitoa taarifa kwa uongozi wa wanakijiji," alisema Mnkondya.

Alisema tukio hilo ni la kusikitisha kwani limekatisha uhai wa mwananchi wake na kuwaasa wakazi wa eneo hilo kuwa makini kipindi hiki cha mvua ambazo zinasababisha mafuriko na mito kujaa maji.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Songwe, ACP Janeth Magomi, alisema jeshi hilo linaendelea na uchunguzi na kwamba baada ya kukamilika litatoa taarifa kamili.

Aliwataka wananchi kuwa makini kipindi cha mvua kutopita kando ya mito usiku, kwani kunaweza kuhatarisha usalama wao na kupoteza maisha.

## Homera atoa kauli kata iliyoko kwenye hifadhi

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, amesema serikali haiwezi kupeleka fedha za miradi ya maendeleo kwenye Kata ya Luhanga iliyoko wilayani Mbarali hadi itakapotoa tafsiri halisi ya Tangazo namba 28 linaloonyesha kuwa kata hiyo iko ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Ruaha.

Homera alitoa kauli hiyo jana kwenye kikao cha kupanga kalenda ya ufundishaji ili kuhakikisha mkoa huo unaendelea kufanya vizuri kitaaluma.

Alisema kwa sasa Kata ya Luhanga inahesabika kuwa iko ndani ya Hifadhi ya Ruaha, hivyo ni ngumu kupeleka miradi ya maendeleo ikiwamo ujenzi wa vituo shikizi hadi hapo serikali itakapo toa tangazo la kuiondoa kata hiyo kwenye (GN namba 28).

"Serikali iliingiza shilingi milioni 160 kwa ajili ya ujenzi wa kituo shikizi katika kata hiyo, lakini baada ya kufanya mawasiliano walipokea maelekezo kwamba zihamishwe zikajenge shule kwingine wakati suala la GN namba 28 litakapotolewa maamuzi na serikali," alisema Homera.

Katika hatua nyingine, Homera aliwapongeza walimu na maofisa elimu wa wilaya zote za mkoa huo kufanya vizuri katika matokeo ya mitihani ya darasa la saba, nne kidato cha pili, nne na sita.

Aliagiza kuandaliwa tafrija ya kuwapongeza walimu na shule zilizofanya vizuri ambapo alisema ifanyike mwezi machi ambapo kila wilaya itafanya shughuli hiyo.

Ofisa Elimu Mkoa wa Mbeya, Ernest Hinju, alisema kalenda ya ufundishaji nchini itasaidia kuondoa tofauti za ufundishaji na kuweka usawa kwani kila shule nchi zitafundisha mtaala wa aina moja na kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Aliongeza kuwa sababu ya kuweka kalenda ya pamoja ya ufundishaji ni kuweka usawa wa ufundishaji baina ya shule na shule au wilaya na wilaya na kwamba kikao cha kujadili mtaala huo kitawahusisha walimu, waratibu elimu na maofisa mkoani humo.

Kwa upande wake Katibu Tawala wa Mkoa wa Mbeya, Dk. Angelina Lutambi, alisema kalenda ya ufundishaji na ujifunzaji utasaidia kuweka usawa wa upatikanaji wa elimu ili kuondoa tatizo ya upimaji wa wanafunzi.

Alisema kalenda hiyo itatoa nafasi kwa walimu kujitathmini kujua wapi walipo na kulisaidia taifa kuangalia mapungufu na mambo gani ya kuboresha ili kukuza taaluma nchini.





# Bil. 32/- za UVIKO kuwanufaisha wajasiriamali

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais (Kazi, Uchumi na Uwekezaji), Mudrik Ramadhan Soraga, amesema kuwa Sh. bilioni 32 zinatarajiwa kutolewa kwa vikundi 2,907 vya wajasiriamali kwa awamu ya kwanza, ambazo zimetolewa na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) kwa ajili ya kupunguza makali ya UVIKO-19.

Alisema kuwa vikundi hivyo 2,907 ndivyo ambavyo vimekidhi vigezo vya kupata mkopo huo kwa ajili ya kuendeleza biashara zao na kujiendesha kiuchumi.

Aliyasema hayo jana wakati akitoa taarifa kwa waandishi wa habari kuhusu kukamilika kwa zoezi la uhakiki wa vikundi hivyo.

"Jumla ya vikundi 3,494 vya wajasiriamali vimehakikiwa ambapo Unguja ni 1,915 na Pemba 1,579, lakini vikundi vinavyokopesheka ni 2,907 na visivyokopesheka ni 587, ambavyo havijatimiza vigezo vinavyotakiwa," alisema Soraga.

Waziri Soraga, alisema wizara yake imepatiwa Sh. bilioni 45 kwa ajili ya kuwawezesha wananchi kiuchumi ikiwamo wajasiriamali, na kwamba hatua ya pili ya kuhakiki vikundi vya wajasiriamali itafuata ili kupata mkopo wa fedha hizo.

Aidha, alisema kuwa fedha hizo zitatolewa kwa utaratibu maalum ambapo fomu za maombi zitatolewa katika ofisi za mkoa kuanzia leo.

Alieleza kuwa katika utoaji wa fedha hizo hakutakuwa na ubabaishaji kama ulivyokuwa katika fedha za mkopo wa mfuko wa JK na AK ambapo watu walizitumia vibaya na kushindwa kufikia malengo.

"Fedha za JK na AK waliopata mkopo huo walizitumia kinyume cha malengo yaliyokusudiwa, wapo ambao waliendа kuoa kwa wale ambao hawajaoa na waliokuwa na wake waliongeza wengine," alisema Soraga.

Alisema serikali itahakikisha inaweka usimamizi mzuri wa fedha hizo ili wajasiriamali wengi kunufaika nazo.

Alieleza kuwa fedha hizo hazitatolewa kwa sababu za kisiasa kama inavyosemwa na baadhi ya watu, na kwamba zimetolewa na serikali kwa dhamira yake ya kuwajali wananchi wake ili kuimarika kiuchumi.



Baadhi ya madereva na makondakta wa daladala zinazofanya safari zake kati ya Iringa Mjini na Mafinga mkoani Iringa wakiwa katika mgomo juzi, kupinga mabasi yanayofanya safari zake nje ya mkoa huo, kuingia stendi ya Ipogolo badala ya stendi ya Igumbilo ambayo ni stendi ya mkoa kama walivyopangiwa. **PICHA: FRANCIC GODWIN**

# Vyuo vikuu vyapewa mbinu kukabiliana na tatizo la ajira

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

MAKAMU wa Kwanza wa Rais, Othman Masoud Othman, amevitaka vyuo vikuu kuanzisha programu maalum za kuwawezesha wajasiriamali kukabiliana na changamoto ya ajira nchini.

Othman aliyasema hayo katika mahafali ya 21 ya kuwatunuku shahada na stashahada jumla ya wahitimu 278 wa Chuo Kikuu cha Abrahaman Al Mumeit kilichoko Chukwani nje kidogo ya mji wa Zanzibar.

Alisema soko la ajira hivi sasa limekabiliwa na changamoto nyingi, ikiwamo ushindani na hivyo kufanya fursa za ajira nazo kuwa na ushindani, hivyo ni vyema vyuo kutengeneza mazingira ya kuwaandaa wahitimu kupata fursa hizo zinazokuwapo.

Hata hivyo, alisema pamoja na changamoto katika soko la ajira, ni vyema vyuo vikuu kuzikabili kwa kupata mtaji wa kuwawezesha vijana kujiajiri na kuajiriwa katika soko la ndani na nje ya Tanzania.

Aidha, alivitaka vyuo vikuu kuendelea kufanya utafiti ili kusaidia utatuzi wa matatizo na kutoa mwelekeo wa maendeleo ya nchi na jamii.

Alisema serikali ya Zanzibar imeelekeza nguvu zake katika sera ya uchumi wa bluu, na kwamba eneo hilo likichangamkiwa litatoa ajira kwa vijana.

Aliutaka uongozi wa chuo hicho kuweka mikakati imara na juhudi endelevu ikiwamo utoaji wa kozi zinazovutia soko la ajira duniani sambamba na kuzalisha wahitimu bora.

Naye Makamu Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Msafiri Mshewa, alisema mtaala wa chuo hicho umefanyiwa mapitio na hivi sasa umeingiza vipengele vya uchumi wa bluu kwa kuzingatia sera ya uchumi wa nchi.

Aliiomba serikali kuwaongezea eneo la ardhi ili kuendeleza majengo mapya yatakayosaidia kuendeleza programu za mafunzo ya TEHAMA na kuzalisha vijana wenye uwezo kulingana na mahitaji ya soko yaliyoko sasa.

Naye Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Simai Mohammed Said, alisema serikali itajitahidi kushirikiana na taasisi mbalimbali

# Waziri aeleza lengo la ujenzi ukuta wa mawe

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Dk. Saada Mkuya, amesema ujenzi wa ukuta wa mawe katika fukwe ya mwambao wa eneo la Msuka una lengo la kudhibiti athari za mmongonyoko.

Aliyasema hayo alipofanya ziara ya pamoja na Kamati ya Baraza la Wawakilishi inayosimamia ofisi za viongozi wakuu wa kitaifa kwenye fukwe za Shehia ya Msuka magharibi mwa kisiwa cha Pemba na kushuhudia ujenzi unaoendelea wa ukuta huo.

Dk. Saada aliwaomba wananchi hasa wavuvi wanaotumia eneo hilo kuhakikisha wanalinda na kutunza ukuta huo kwa maslahi yao na vizazi vijavyo pamoja na kuchukua tahadhari katika kulinda rasilimali za bahari na viumbe hai kwa kuepuka matumizi ya mifuko ya plastiki na kutotupa ovyo taka za plastiki.

Alisema shughuli zao za kijamii na uvuvi ziendelee bila ya kuathiri ukuta huo, ambapo serikali imechukuwa jitihada kubwa katika kulinda na kuhifadhi mazingira ya eneo hilo yasiathirike pamoja na kuondoa uwezekano wa athari za kiuchumi na kijamii zilizokuwa zimejitokeza.

Naye Mwenyekiti wa Kamati ya Baraza la Wawakilishi inayosimamia ofisi za viongozi wakuu wa kitaifa, Hassan Hafidh, aliipongeza Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa usimamizi mzuri uliowezesha kujengwa kwa ukuta huo uliozingatia muda na mahitaji ya wavuvi na wananchi wa eneo hilo

Mhandisi Atanasi Abdul Malik Said, kutoka Ofisi ya Wakala wa Majengo, alisema ujenzi huo umeshafikia urefu wa mita 500 na shughuli zinazoendelea kwa sasa ni ujenzi wa nguzo na kuweka mkanda kwenye ukuta kwa ajili ya kuimarisha na kuweka nguzo zaidi ya 120 kwa ukuta wote wa mita 500.

Akiwakilisha wavuvi na wachuuzi wa eneo hilo, Khamis Suleiman Amour, aliishukuru serikali na uongozi uliofika kwa kutimiza ahadi na kuahidi kuwa watakuwa walinzi wema wa eneo hilo ili lisiharibiwe na harakati za kibinadamu.

Katika kufanikisha ujenzi wa ukuta huo, jumla ya Sh. milioni 300 zilipangwa kutumika ambapo hadi kufikia Desemba 2021, Sh. milioni 200 zilikuwa zimetumika, na ujenzi unatarajiwa kukamilika Machi mwaka huu.

# Walengwa TASAF waelezea unafuu kuwezeshwa matibabu

**Na Elizabeth Zaya, HANDENI**

WALENGWA wa Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini, unaosimamiwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), wamesema mpango huo umewasaidia kwa kiwango kikubwa kupata matibabu kwa urahisi wanapopatwa na shida ya kiafya tofauti na ilivyokuwa awali kabla ya kuingizwa katika mpango huo.

Walitoa kauli hiyo kwa nyakati tofauti wilayani Handeni mkoani Tanga, walipotembelewa na maofisa wa TASAF kutoka makao makuu.

Walisema kupitia mpango huo umewawezesha kukata bima ya afya na hivyo kupata fursa ya kupata huduma ya matibabu kwa urahisi wanapopatwa na shida ya kiafya.

"Mwanzoni kabla ya kuingia kwenye mpango huu wa TASAF tulikuwa hatuna uwezo wa kupata pesa ya kukatia bima ya afya, kwa hiyo tulikuwa tunapata shida kupata matibabu, sana sana tulikuwa tunakwenda dukani tunanunua panado tunameza, yaani ni Mungu tu ndiye alikuwa anasaidia kwa neema zake tunapona," alisema Dorkasi Mganga, mkazi wa mtaa wa Kidereko, Handeni.

"Tulipoingizwa kwenye mpango tulishauliwa kwamba tutumie pesa kidogo tunayopata tukate bima ili tusipate shida ya matibabu, kwa kweli tangu tulipofanya hivyo imetusaidia sana. Nakumbuka mwanzoni kabisa wakati nimeingizwa TASAF nililegalega kukata bima, lakini bahati mbaya mwanangu akawa ameugua, yaani nilijilaumu sana, nilitumia Sh.17,000 kumtibia na mimi mwenyewe nikaugua nikatumia Sh.18,000 na tangu hapo nikaona umuhimu wa bima, nilienda haraka kuitafuta. "

Fatma Muya, mkazi wa mtaa wa Kileleni Kata ya Vibaoni, Handeni, alisema yeye baada ya kuingizwa kwenye mpango huo wa kunusuru kaya maskini, alikata bima kwa ajili yake na watoto wake wanne ambayo imekuwa ikiwasaidia kupata matibabu. "Mimi watoto wangu siyo wakubwa sana, kwa hiyo kwenda hospitali huwa ni mara kwa mara, na kabla ya kuanza kupata pesa hii ya TASAF ilikuwa ni vugumu kulipia gharama kila wanapougua, kwa hiyo wakati mwingine nilikuwa nashindwa nanunua dawa ya kutuliza maumivu tu, lakini kupitia mpango huu sina wasiwasi tena, wote wana bima," alisema Muya.

"Wapo wenzetu tulionao kwenye mpango ambao wanaona kuchukua pesa kidogo wakate bima wanaona wanaimaliza, mimi nawashauri wakate kwa sababu ukiugua kama huna hiyo unatumia gharama kubwa."




Mshindi wa promosheni ya Vodacom "Show Love, Tule Shangwe", Veronica Kalamu (wapili kulia) mkazi wa Runzewe akipokea mfano wa hundi ya shilingi milioni moja kwa Mkuu wa Mauzo wa Vodacom Kanda ya Ziwa, Ayubu Kalufya (kulia), katika hafla iliyofanyika viwanja vya Phantom, mjini Kahama, mkoani Shinyanga jana. Wengine ni maofisa wa kampuni hiyo. Msimu huu wa sikukuu Vodacom inatoa zawadi kwa wapendanao ambapo wateja wanaweza kununua bando na kutumia huduma ya M-Pesa kwa kupiga *149*01#

## Waziri awapa mbinu ya ajira wahitimu wa utalii

**Na Christina Mwakangale**

NAIBU Waziri wa Maliasili na Utalii, Mary Masanja, amesema wahitimu wa Chuo cha Utalii cha Taifa (NCT), mwaka 2020/21, kutumia ujuzi walioupata kwa kujiajiri, badala ya kwenda kuwa mzigo kwa jamii na taifa.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam, kwenye mahafali ya 19 ya chuo hicho, kwa wahitimu wa ngazi ya astashahada na stashahada 541, Masanja alisema kutokana na uhaba wa ajira wahitimu hao wasisubiri ajira za serikali pekee.

"Chagua moja kuajiriwa, au kujiajiri, usiende kuwa mzigo kule uendako. Mkawe wabunifu. Kwa miaka 60 ya Uhuru, hatujawahi kuwa na vazi rasmi, muwe wabunifu wa vazi hili ili kuitangaza Tanzania," alisema Masanja.

Alibainisha kwamba fursa zinazohisiana na sekta hiyo, zipo kuanzia ngazi za chini, kwenye wilaya mikoa na kitaifa, na kwamba changamoto iliyoko sasa ni uhaba wa wataalamu kuandaa matukio ya hafla mbalimbali.

Alisema serikali itaendelea kuimarisha huduma zinazotolewa na sekta hiyo, ikiwamo mafunzo ya chuo hicho ingawa ugonjwa wa UVIKO-19 ulisababisha kuyumba kwa shughuli za kitalii na uchumi.

"Ili kukabiliana na UVIKO-19, IMF ilitoa fedha kwa ajili ya kukabili sehemu ya changamoto za ugonjwa huu, kuboresha miundombinu, kutoa mafunzo na kuiinua sekta ambayo ni kati ya zilizoathiriwa na janga hili," alisema Masanja.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa NCT, Dk. Shogo Mlozi, alisema idadi ya wahitimu inaongezeka kila mwaka na kwamba mkakati ni kutoa mafunzo ngazi ya shahada.

Alisema katika mwaka wa masomo 2020/21, kati ya wahitimu 542, wapatao 204 ni kutoka kampasi za Bustani, 270 na Temeke mkoani Dar es Salaam, pia 67 kutoa Arusha.

Alisema wahitimu hao wa mwaka wa masomo 2020/21 wamehitimu mafunzo ya Uratibu wa Matukio, Huduma za Mapokezi, Chakula na Ufuaji, Utunzaji Vyumba, Ukarimu, Uokaji, Mapishi na Uongozaji, Usafirishaji Watalii.

# Kagera yatenga bajeti ya bil. 346/-

**Na Restuta Damian, BUKOBA**

MKOA wa Kagera umepitisha makisio ya bajeti ya Sh. bilioni 346 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo kwa mwaka 2022/2023.

Hatua hiyo ilibainishwa mwishoni mwa wiki na Katibu Tawala (mipango na usaidizi wa uratibu) mkoani humo, Nestory Bwana, wakati akisoma taarifa ya makisio ya bajeti hiyo kwenye kikao cha Kamati ya Ushauri ya Maendeleo ya Mkoa (RCC).

Bwana alisema fedha hizo zimeongezeka kutoka Sh. bilioni 294 kwa mwaka 2021/2022 na kufikia Sh. bilioni 346 ambazo ni makusanyo ya vyanzo vya ndani na michango ya wadau wa maendeleo.

"Kwa miaka mingi kidogo fedha za maendeleo ilikuwa ikitoka kwa asilimia ndogo, lakini mwaka huu, tumefika nusu mwaka na tukiwa asilimia 50 yaani imeongezeka kidogo," alisema Bwana.

Aidha, alisema shughuli zitakazofanyika ni pamoja na kuendeleza miradi mbalimbali ya kimkakati ukiwamo ujenzi wa kituo cha magari ya mizigo kinachoendelea kujengwa katika Nata Nyakanazi wilayani Biharamulo.

"Mfano mradi wa kituo cha magari ya mizigo inayotoka nchi jirani na kuingia mkoani humu pia kutoa nchini kwenda nje ambacho ujenzi wake umefikia asilimia 95," alisema Bwana.

Aliongeza kuwa kwa mwaka 2021/2022 shughuli mbalimbali zilifanyika na kuanza kutoa huduma zikiwamo ujenzi wa vyumba vya madarasa kwa shule za sekondari.

"Tuliangalia hapa hadi kufikia Desemba mwaka 2021 miradi ya ujenzi wa vyumba vya madarasa vilikuwa vimekamilika na wanafunzi waliofungua shule mwezi huu wanavitumia," alisema Bwana.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya Bukoba, Murshid Ngeze, alisema endapo fedha hizo zitaidhinishwa na TAMISEMI na viongozi kuzisimamia vizuri zitasaidia kuleta maendeleo mkoani.

Ngeze alisema yapo maeneo ambayo yanahitaji miradi ya kuendelezwa na kunufaisha wananchi wa vijijini ili waweze kupiga hatua.

HABARI KIMATAIFA

## Miaka miwili yapita tangu China ilifungie jiji la Wuhan

**Beijing, CHINA**

JANA imetimia miaka miwili, tangu China ilifungie jiji la Wuhan ili kudhibiti mlipuko wa virusi vya corona.

Kufungiwa kwa Wuhan, jiji lililoko katika Jimbo la Hubei kulikuja wakati dunia ilipothibitisha kwa mara ya kwanza mlipuko wa ugonjwa wa Uviko-19 katika jiji hilo.

Hatua hiyo ilidumu kwa miezi miwili na nusu.

Serikali kuu imekuwa ikiendeleza sera ya zero - Covid, yaani ya kutokuwa na ugonjwa huo kabisa, ili kuzuia kusambaa kwa virusi.

Sera hiyo inajumuisha upimaji mkubwa wa kutumia kipimo cha PCR pamoja na kufungwa kwa maeneo ambayo maambukizi yamekuwa yakiripotiwa.

Desemba mwaka jana, mamlaka zilitekeleza hatua ya kufungia mji wa Xi'an ulioko katika Jimbo la Shaanxi.

Jiji hilo lina idadi ya watu takribani milioni 13 na kufanya hatua hiyo kuwa sawa na ile ya Wuhan kwa idadi ya watu walioathirika.

Hatua hiyo ya kufungia mji huo, bado inatekelezwa katika baadhi ya sehemu za Xi'an.

Mamlaka pia zimefunga baadhi ya maeneo ya jiji la Beijing, mji wa jirani wa Tianjin na kwingineko baada ya visa vya virusi vya corona aina ya Omicron kugundulika huko.

Maofisa hivi sasa wanahangaika kudhibiti maambukizi kabla ya mashindano ya olimpiki ya msimu wa baridi ya Beijing, ambayo sherehe zake za ufunguzi zitafanyika Februari 4.

**NHK**

# Risasi zarindima kambi ya jeshi

**Ouagadougou, BURINA FASO**

MILIO mizito ya risasi imesikika kwenye kambi ya jeshi katika mji mkuu wa Burkina Faso, Ouagadougou mapema jana, asubuhi.

Waziri wa Ulinzi Burkina Faso, Jenerali Bathelemy Simpore, amekanusha uvumi kwamba, Rais Roch Marc Kabore, amezuiliwa baada ya milio ya risasi kwenye kambi kadhaa za jeshi.

Amesema, sababu ya kupigwa risasi kwenye kambi ya wanajeshi bado haijafahamika

Serikali ya Burkina Faso, ilithibitisha juu ya milio ya risasi kusikika kwenye kambi kadhaa nchini humo, ingawa ilikanusha kutokea mapinduzi ya kijeshi.

Kwa mujibu wa Shirika la habari la Reuters, watu waliozungumza nao walisema, milio hiyo ilianza alfajiri na kuendelea hadi mapema asubuhi ya jana kwenye kambi ya Sangule na Lamizano.

Miji hiyo ambayo ni makao makuu ya maofisa wa jeshi na gereza ambalo baadhi ya wafungwa wake ni askari waliohusika katika jaribio la mapinduzi la mwaka 2015 ambalo halikufanikiwa.

Mmoja wapo ni Jenerali Gilbert Diindere, aliyekuwa mshirika mkuu wa rais wa zamani wa Burkina Faso Blaise Compaore aliyepinduliwa mwaka 2014. Mapema mwezi huu wanajeshi wanane walikamatwa kutokana na tuhuma za kupanga njama dhidi ya serikali. **DW**



Wanajeshi wa Jeshi la Ukraine wakiendelea na mafunzo kwenye jiji la Kyiv nchini humo, mwishoni mwa wiki. Makumi ya wakazi wa Ukraine wameambiwa wajiunge na jeshi hilo wiki chache zilizopita ili kuongeza nguvu kazi. **PICHA: REUTERS**

# Mkuu wa jeshi Ujerumani ajiuzulu

**Berlin, UJERUMANI**

MKUU wa Jeshi la Wanamaji Ujerumani, Kay-Achim Schoenbach, amejiuzulu baada ya kutoa matamshi yenye utata kuhusu mzozo wa Ukraine.

Schoenbach, amejiuzulu Jumamosi usiku baada ya kusema kwamba Rais wa Urusi, Vladmir Putin anahitaji heshima na kwamba rasi ya Crimea kamwe haitorejea kwa Ukraine.

"Anachohitaji sana ni heshima. Na kumpa mtu heshima ni gharama ndogo. Iwapo ingeulizwa, ni rahisi kumpa heshima anayoidai na pengine anastahili heshima hiyo," alifafanua Schoenbach.

Schönbach aliyatoa matamshi hayo siku ya Ijumaa akiwa ziarani nchini India, ambayo hayakuifurahisha Ukraine na kusababisha Wizara yake ya Mambo ya Nje kumuita balozi wa Ujerumani, Anka Feldhusen kuelezea kwamba haikubaliani na matamshi hayo.

Schoenbach alisema amemwomba Waziri wa Ulinzi wa Ujerumani, Christine Lambrecht, kumruhusu aachane na majukumu yake mara moja na amethibitisha kuwa waziri huyo amelikubali ombi lake.

Matamshi hayo aliyatoa baada ya Urusi kupeleka wanajeshi 100,000 katika mpaka wake na Ukraine na kusababisha wiki kadhaa za mazungumzo ya kidiplomasia kuzuia uhasama kuzuka.

Hata hivyo, Urusi ilikanusha kuivamia Ukraine kijeshi, ingawa ilitaka kuhakikishiwa na Jumuiya ya Kujihami NATO kwamba haitoingia kwenye ardhi ya Ukraine, wala haitoendelea kujitanua katika upande wa mashariki ya Ulaya.

Akizungumza katika Taasisi ya Mafunzo ya Ulinzi na Utafiti ya Manohar Parrikar, Schoenbach alisema anaiona China kuwa ndiyo kitisho kikubwa na kwamba Ujerumani na India kwa pamoja zinamuhitaji Urusi kwa lengo la kupambana na China.

Kuhusu mzozo kati ya Urusi na Ukraine, Schoenbach alisema Rasi ya Crimea imetoweka na ukweli ni kwamba haiwezi kamwe kurejea Ukraine.

Matamshi yake yanagusia hatua ya Urusi kuinyakuwa Rasi ya Crimea mwaka 2014, moja ya matukio yaliyoanzisha uhasama uliodumu kwa muda mrefu.

Msemaji wa Wizara ya Ulinzi ya Ujerumani amesema wizara hiyo imejitenga na maoni ya Schoenbach na kwamba matamshi hayo hayafungamani na msimamo wa wizara.

Wizara hiyo ilisema, Schoenbach anapaswa kujieleza kwa mkuu wake, Inspekta Jenerali Eberhard Zorn na kwamba serikali ya muungano ya Ujerumani italijadili suala hilo Jumatatu.

Kwa upande wake Schoenbach aliomba radhi kupitia ukurasa wake wa Twitter, akisema matamshi yake yalikuwa kosa la wazi na hakuna haja ya kubishana.

"Matamshi yangu ya sera ya utetezi wakati wa kikao na taasisi ya India yaliakisi maoni yangu binafsi kwa wakatu huo," aliandika Schoenbach. Amesema matamshi yake hayaakisi msimamo wa wizara ya ulinzi.

Wakati huo huo, Waziri wa Mambo ya Nje wa Ukraine, Dmytro Kuleba, aliikosoa hatua ya Ujerumani kukataa kupeleka silaha nchini humo na kuitaka Ujerumani kuacha kuudhoofisha umoja na kumhimiza Rais Putin, huku kukiwa na hofu ya Urusi kuivamia Ukraine.

**DW**

HABARI MICHEZO

# MBEYA CITY: SISI NAFASI YA 3 UBINGWA NI SIMBA, YANGA

**Na Saada Akida**

LICHA ya kuwa katika nafasi nzuri kwenye mbio za ubingwa wa Ligi Kuu Bara, Kocha Mkuu wa Mbeya City, Mathias Lule, ameweka wazi kuwa timu yake haina uwezo wa kutwaa taji hilo, lakini wana kila sababu ya kumaliza nafasi tatu za juu mwisho wa msimu huu.

Mbeya City imecheza michezo 13, ikishinda mitano, sare saba na imepoteza mmoja, hivyo kujikusanyia pointi 22 ikiwa nafasi ya tatu chini ya Simba yenye alama 25 na vinara Yanga pointi 32 ambazo zimeshuka dimbani mara 12.

Akizungumza na gazeti hili jana, Lule alisema kulingana na uwezo wa timu yake, hataingia katika vita vya timu kubwa za Simba na Yanga kupambania mbio za ubingwa, ila anaweza kupambana kujihakikishia kubaki nafasi ya tatu.

Alisema anapambana kuhakikisha wanafanya vizuri katika michezo yao ijayo, lengo kubwa likiwa ni kuendelea kuvuna pointi ili kumaliza katika nafasi ya tatu walioko kwa sasa katika msimamo wa ligi hiyo.

"Ligi imekuwa na ushindani mkubwa pia kuna ugumu kwa sababu kila timu imejipanga vizuri, nahitaji kuona kikosi changu kinaendelea kufanya vizuri katika kila mechi ili kufikia malengo hayo.

"Nina imani wachezaji wangu wakiwa makini na kufanya majukumu yao kwa kufuata kile ninachowapa mazoezini na kukionyesha kwenye mechi, tuna uwezo mkubwa wa kumaliza katika nafasi hiyo, suala la ubingwa hatuwezi kuingia katika vita hivyo kwa msimu huu.

"Kama nilivyosema awali msimu huu tumekuja kivingine, tunataka kuchafua watu hatujali tunakutana na timu yenye ukubwa upi ama aina ya wachezaji waliokuwa nao, kikubwa tunahitaji pointi iwe ugenini au nyumbani," alisema Lule.

Alisema ili kutimiza malengo hayo anahakikisha anawapa mbinu na ufundi ili kupata matokeo chanya kwenye michezo iliyoko mbele yao dhidi ya Yanga na Namungo FC, watakapokuwa ugenini.

Mbeya City ina kibarua kigumu ugenini dhidi ya wenyeji wao Yanga, mchezo utakaopigwa Februari 5, mwaka huu, katika Uwanja wa Benjamini Mkapa, Dar es Salaam.

MRS WORLD 2021...




Mshindi wa taji la Mrs India-World 2021', Namrata Shah akizungumza kwenye hafla ya kupongezwa iliyoandaliwa na 'Incredible Naari', jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki na kuhudhuriwa na wanakikundi wa jukwaa hilo. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

# Mrs India-World 2021 atoa siri ya ushindi

**Na Christina Mwakangale**

MSHINDI wa taji la Mrs India-World 2021, Namrata Shah, ameelezea namna alivyotwaa taji hilo, akisema kujiamini, tabasamu na kujibu maswali kwa ufasaha ni sababu ya kuwashinda washiriki takriban 100 kutoka nchi tofauti duniani.

Shah, ambaye ni mkazi wa Dar es Salaam, ametwaa taji hilo la urembo, lililoandaliwa na Skywalk Productions, mwishoni mwa mwaka jana, jijini Delhi nchini India.

Akizungumza na Nipashe, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, kwenye hafla ya kumpongeza iliyoandaliwa na Incredible Naari, Shah alisema palipo na nia hakuna kinachoshindikana duniani na kwamba amekuwa akiamini hivyo tangu akiwa mdogo.

"Mbali na shughuli za urembo pia ninaungana na wanawake wenzangu ili kuwawezesha katika masuala ya kijamii na huduma za kiutu.

"Ninafanya kazi bila kuchoka katika masuala ya kijamii hasa kwa watoto wasiojiweza, naamini hakuna sababu kubwa zaidi kuliko ubinadamu," alisema Shah.

Aidha, kwenye hafla hiyo iliyoandaliwa na Jukwaa la Wanawake wa Kipekee, yalikuwapo mashindano ya kumpata mshindi kutoka katika jukwaa hilo, huku Geeta Kumar akivikwa taji hilo la 'Incredible Naari 2022'.

Mmoja wa waandaaji wa hafla hiyo, Jaya Chowdary, alisema jukwaa hilo linawaunganisha wanawake wenye shughuli tofauti mtandaoni, ikiwamo wajasiriamali, wabunifu, matabibu pamoja na kutoa msaada kwa makundi maalum kila mwaka.

"Incredible Naari ina maana wanawake wa kipekee, ambao tunakutana mtandaoni duniani. Tuliopo hapa Dar es Salaam huwa tunakutana na kuchangishana kusaidia yatima, kuwawezesha wanawake, wanakikundi wenye fani ya udaktari hutoa ushauri bure," alisema Jaya.

"Muhimu zaidi katika hili jukwaa la 'Incredible Naari' linawapa wanawake fursa ya kuwa wao wenyewe na ndivyo tunavyohitaji leo."

# Ajibu aanza kutupia, abadili jina Azam FC

**Na Adam Fungamwango**

KIUNGO mshambuliaji mpya wa Azam FC, aliyesajiliwa na timu hiyo siku chache kabla ya dirisha dogo la usajili kufungwa Januari 15, mwaka huu, akitokea Simba, amefunga bao la kwanza kwenye timu yake mpya, huku akitoa sababu ya kubadilisha jina kwenye jezi yake kutoka Ajibu na kuandika Migomba.

Kwenye Uwanja wa Nelson Mandela mjini Sumbawanga, Ajibu alikuwa mmoja wa wafungaji wa mabao manne ambayo Azam iliishindilia Prisons kwenye mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Ilikuwa ni mechi ya pili kwa mchezaji huyo wa Ligi Kuu Tanzania Bara tangu kujiunga na timu hiyo, licha ya kucheza michuano ya Kombe la Mapinduzi Zanzibar, mechi ya kwanza ikiwa ni dhidi ya Mbeya Kwanza iliyochezwa Januari 18 na Azam kushinda bao 1-0 katika Uwanja wa Sokoine, jijini Mbeya.

**"Mashabiki wa Azam wa tarajie makubwa zaidi kwa sababu tunazidi kucheza na tunataka kufikia malengo . Mwanzoni ilinisumbua mfumo, lakini sasa nimean za kuelewana na wachezaji wenzangu," alisema mchezaji huyo ambaye soka lake liliinukia kwenye kikosi cha pili cha Simba, lakini ak iwa amewahi pia kuichezea Yanga.**

Kuhusu kubadili jina kwenye jezi yake kutoka Ajibu alipokuwa kwenye klabu ya Simba na kuandika Migomba alipojiunga na Azam, alisema hayo yote ni majina yake, hivyo ana uwezo wa kuchagua muda gani wa kutumia jina lipi.

"Ni kweli, huku Azam nimeandika Migomba, haya yote ni majina yangu, kwa hiyo wala si kitu cha ajabu, mimi mwenyewe tu naamua kuchagua jina gani na kwa muda gani, au kwenye timu gani, ndiyo maana huku nimeamua kuandika hivi," alisema.

HABARI MICHEZO

ZISIKUPITE

### ALVAREZ ATAKIWA CITY
KLABU ya Manchester City ipo tayari kuipiku Real Madrid katika mbio za kumsajili mshambuliaji wa River Plate, Julian Alvarez. Muargentina huyo mwenye umri wa miaka 21, amepewa jina la Sergio Aguero mpya, huku Barcelona na Bayern Munich pia wakimtaka. ***(Star)***

### TARKOWSKI KUTUA NEWCASTLE
NEWCASTLE United wana matumaini ya kumsajili beki wa Burnley, James Tarkowski, huku klabu yake ikiwa tayari kuchukua ofa ya kumnunua nyota huyo mwenye umri wa miaka 29. ***(Sun)***

### VLAHOVIC ANUKIA ARSENAL
ARSENAL wamewasilisha ombi la euro milioni 70 ili kumsajili mshambuliaji wa Fiorentina, Dusan Vlahovic. Mshambuliaji huyo wa Serbia mwenye umri wa miaka 21, amefunga mabao 17 katika mechi 21 za Serie A msimu huu.(Tutti Mercato)

### CALVERT-LEWIN KUTUA WEST HAM
KLABU ya West Ham wanataka kumsajili mshambuliaji wa Everton na England, Dominic Calvert-Lewin, lakini Everton inataka pauni milioni 60 kwa ajili ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24. ***(Sun)***

### RAMSEY HUYOOO BURNLEY
KLABU ya Burnley wanataka kumsajili kiungo wa kati wa Juventus, Aaron Ramsey mwenye umri wa miaka 31, kwa mkopo hadi mwisho mwa msimu. Kocha wa Juve Massimiliano Allegri amethibitisha kuwa mchezaji huyo wa Wales ataondoka katika klabu hiyo mwezi huu***. (Sun)***

### ANCELOTTI KUMBAKIZA HAZARD
KOCHA wa Real Madrid, Carlo Ancelotti anasema Eden Hazard yuko mbioni kusalia katika klabu hiyo. Winga huyo wa Ubelgiji mwenye umri wa miaka 31, amehusishwa na kurejea Ligi Kuu ya England Januari hii. ***(Mail)***

### BENTANCUR AMULIKWA VILLA
KLABU ya Aston Villa ina nia ya kumsajili kiungo wa kati wa Juventus mwenye umri wa miaka 24, Rodrigo Bentancur. Mchezaji huyo, raia wa Uruguay amecheza mechi 18 za Serie A msimu huu. ***(Mail)***

### CARLOS KUPELEKWA SOKONI
WAWAKILISHI wa mlinzi wa Sevilla, Diego Carlos wanajaribu kuishawishi klabu hiyo kumuuza kwa Newcastle. Newcastle inayomtaka Mbrazili huyo mwenye umri wa miaka 28, huku klabu hiyo ya Hispania ikitaka takriban pauni milioni 60. ***(90 min)***

### TRAORE KUTUA SPURS
WEST Ham imejiondoa kwenye mbio za kumsajili winga wa Wolves, Adama Traore baada ya kuambiwa raia huyo wa Hispania mwenye umri wa miaka 25, anasaini kwenda Tottenham Hotspur. ***(Football Insider)***

### SOSA WAMFUATA CHELSEA
CHELSEA wameingia kwenye kinyang'anyiro cha kumnunua mlinzi wa kushoto wa Stuttgart, Borna Sosa mwenye umri wa miaka 24. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Croatia alilengwa na Aston Villa mapema wakati wa dirisha la usajili, huku Inter Milan pia ikimtaka. ***(Sky Deutschland's Marc Behrenbeck on Twitter-in German)***

### LIVER YAJITOA KWA ZAKARIA
LIVERPOOL imejiweka kando katika mbio za kumsajili kiungo wa kati wa Borussia Monchengladbach, Denis Zakaria. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Uswisi mwenye umri wa miaka 25, awali alihusishwa na kuhamia Anfield. ***(Liverpool Echo)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# IBRAHIMOVIC: MBAPPE NENDA TU REAL MADRID

●●●Aliniomba ushauri, ndio nilimwambia kama ningekuwa mimi ningekwenda Real...

**PARIS, Ufaransa**

ZLATAN Ibrahimovic amemshauri Kylian Mbappe kuondoka Paris Saint-Germain na kujiunga na Real Madrid baada ya mshambuliaji huyo kumuomba ushauri.

Mbappe alipewa ofa ya fedha kubwa kuhamia Madrid kipindi cha dirisha la majira ya joto lililopita na hivi karibuni aliomba ruhusu ya kuondoka PSG.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa mkataba wake wa sasa unamalizika mwishoni mwa msimu huu na amekuwa akihusishwa sana na mpango wa kuhamia kule Santiago Bernabeu.

Ametumia misimu sita akiwa na PSG, huku msimu wa kwanza akitua kwa mkopo kutoka Monaco.

Na sasa Ibrahimovic straika wa zamani wa PSG anaamini kuwa ni wakati sasa wa Mbappe kuondoka na kwenda kwenye ligi mpya.

"Ni Kylian pekee anaweza kujibu kuhusu wapi pa kwenda. Inategemea nini anataka, na nini anachokitaka," alisema Ibrahimovic akiiambia L'Equipe.

"Mimi ningeshaondoka. Lakini kama ningekuwa PSG, ningejaribu kumbakisha. Yeye ndio mtu wa kuamua. PSG inataka kumbakiza, lakini je, anataka kuondoka?

"Pia nafikiri kuna klabu nyingine zinamtaka yeye: Kama wewe ni kocha, na una nafasi unaweza kumchukua Mbappe.

"Aliniomba ushauri, ndio nilimwambia kama ningekuwa mimi ningekwenda Real."

Ibrahimovic alitumia misimu minne akiwa na PSG na alifunga mabao 156, akipitwa na Edinson Cavani pekee aliyefunga mabao 200.

SportPesa | LIVE IN PLAY

MECHI KALI
GUINEA
VERSUS
GAMBIA
1 | 2.17
X | 2.93
2 | 3.72

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# GUARDIOLA AWEKA REKODI YA POINTI 500 KWA HARAKA EPL



**MANCHESTER, England**

PEP Guardiola amekuwa kocha wa kwanza kufikisha pointi 500 kwa haraka zaidi kwenye Ligi Kuu England wakati Manchester City ikitoka sare ya bao 1-1 na Southampton, Jumamosi.

Kocha huyo kutoka Katalunya ambaye aliiongoza Man City kwa mara ya kwanza Agosti 2016, alifikia idadi hiyo muhimu katika mechi 213 - ikiwa 18 pungufu ya Jose Mourinho.

Jurgen Klopp ndiye anayefuata kwenye orodha hiyo akiwa amefikisha pointi 500 katika michezo 236 akiwa na Liverpool, huku kocha wa Man United, Alex Ferguson akihitaji mechi 242 kufanya hivyo.

Arsene Wenger (mechi 249) anamaliza tano bora, na Rafael Benitez (267), David Moyes (340), Martin O'Neill (351), Mark Hughes (367), Sam Allardyce (386), Harry Redknapp (392) na Steve Bruce (441) pia wamefika pointi 500.

City wamechukua pointi nyingi dhidi ya Arsenal (34) kuliko mpinzani yeyote chini ya Guardiola, wakifuatiwa na Burnley, West Ham (zote 31), Leicester City na Watford (zote 27).

Mabingwa hao watetezi wa Ligi England walipoteza pointi kwa mara ya kwanza katika mechi 13 baada ya kufungwa 2-0 nyumbani na Crystal Palace Oktoba 30, na kuwaacha kwa pointi 12 Liverpool walio nafasi ya pili wakiwa wamecheza michezo miwili zaidi.

Kyle Walker-Peters aliifungia Southampton bao la kuongoza, lakini Aymeric Laporte akasawazisha.

# Ancelotti kumbakiza Hazard

**MADRID, Hispania**

CARLO Ancelotti amesema Eden Hazard yupo kwenye mipango ya Real Madrid kwa ajili ya msimu ijayo wakati nyota huyo wa Ubelgiji akionyesha ishara ya kurudi kwenye kiwango chake.

Alifunga bao katika muda wa ziada kuwapelekea Madrid kwenye robo fainali ya Copa del Rey dhidi ya Elche wiki hii, akiwa ametoka kutoa asisti kwa Marco Asensio kwenye ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Alcoyano katika mechi iliyopita.

Inamaanisha kwamba, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31, amehusika kwenye mabao mengi katika mechi mbili zilizopita na amekuwa akianza kwenye kikosi hicho.

Hazard ameripotiwa kukataa kuondoka klabuni hapo mwezi huu, akizipiga chini ofa kutoka Newcastle United, na Ancelotti anataka kumbakiza kwa muda mrefu.

"Ndio, yupo kwenye mipango kwa msimu ujao," alisema kocha huyo wa Madrid kabla ya mchezo wa jana Jumapili.



CHEZA USHINDE KASINO

JISAJILI CHEZA SHINDA

# SIMBA YAKIRI UBUTU KWA MASTRAIKA WAKE

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kucheza mechi mbili dhidi ya Mbeya City Jumatatu iliyopita ikichapwa bao 1-0, huku na Mtibwa Sugar juzi, Jumamosi ikitoka suluhu, klabu ya Simba imekiri kuna shida kwenye eneo lake la ushambuliaji.

Ofisa Habari wa klabu ya hiyo, Ahmed Ally, amesema kuwa tayari timu hiyo imecheza mechi mbili ambazo ni sawa na dakika 180 bila kufunga bao lolote, kitu ambacho si cha kawaida kwenye timu kubwa kama ya Simba.

"Matokeo si mazuri sana, tulitaraji kushinda na Mtibwa wamekuwa bora kwenye mikakati yao, wamefanikiwa tusiwafunge na hiki ndicho walichodhamiria kama ambavyo timu zote ndogo zinavyocheza na kubwa. Ila sisi wenyewe tunapaswa kujiuliza zaidi tunakwama wapi kwa sababu tumecheza mechi mbili, tumemaliza dakika 180 pasipo kupata bao. Simba si timu ya kucheza dakika zote hizo bila kupata bao, una Mugalu (Chris), Bocco (John), Kagere (Meddie), kwa hiyo niseme pamoja na mambo yote ya uwanja kuwa na maji, lakini mwisho wa siku niseme kuna shida kwetu ambayo ni lazima tuiangalie," alisema Ahmed.

Alisema kutokana na hali hiyo, Kocha Mkuu, Pablo Franco na benchi lake la ufundi watakaa na kuhakikisha mechi zinazokuja wanarekebisha makosa ya timu kushindwa kupata mabao, wakati tayari upande wa nafasi ya ulinzi kumeimarika kwani hakujaruhusu bao lolote kwenye mechi dhidi ya Mtibwa Sugar.

"Lazima tukae na tuliangalie na tulitatue suala hili, watu tunao, kwa hiyo ni namna gani tu mwalimu na benchi lake watakwenda kurekebisha makali ya mastraika wetu, niwatoe hofu wanachama na mashabiki wa Simba kuwa bado mapema, nafasi ya ubingwa iko wazi, kwa sababu hii ni sare ye nne na ndiyo kwanza ni mechi ya 12," alisema.

Naye Kocha Msaidizi wa Mtibwa Sugar, Idd Salim, alisema kuwa mpango mkakati walioufanya kwa Simba vilevile wataufanya siku wakicheza na Yanga kwenye uwanja huo.

"Mipango yetu imetimia nusu, tulijiandaa tushinde, lakini tumepata pointi moja tunashukuru Mungu, tulijua kuwa mechi itakuwa ngumu kwa sababu ya ubora wa wapinzani wetu, ina wachezaji bora wa ndani na nje ya nchi, benchi bora la ufundi, pia inaiwakilisha nchi kwenye michuano ya kimataifa, hivyo tulitafuta ubora wao tukaudhibiti na udhaifu wao tukautumia. Hata mechi dhidi ya Yanga kwenye uwanja huu tutaandaa mkakati huo huo, japo kwa sasa ipo vizuri, haijapoteza na inaongoza ligi, lakini kwa sasa tunawafanyia kazi ya kuwafuatilia ili tujue jinsi ya kuwadhibiti," alisema.

# Prisons wamfungua mdomo Kocha Azam

**Na Saada Akida**

KAIMU Kocha Mkuu wa Azam FC, Abdihamid Moallin, amesema matokeo aliyoyapata dhidi ya Tanzania Prisons yanampa matumaini makubwa ya kufanya vizuri zaidi katika Ligi Kuu Tanzania Bara na Kombe la Shirikisho la Azam (ASFC), maarufu FA Cup.

Azam FC juzi iliibuka na ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya Tanzania Prisons katika Uwanja wa Nelson Mandela mjini Sumbawanga.

Akizungumza na gazeti hili jana, Moallin alisema timu yake imekuwa na mabadiliko makubwa katika uchezaji yanayowapa matokeo mazuri ikiwamo katika mchezo huo dhidi ya Tanzania Prisons, jambo ambalo liwapa taswira nzuri kwa mechi zao zijazo.

"Mashambulizi ya kujibu pindi tukipata umiliki wa mpira kwa ujumla ni kiwango kizuri sana, kilichoonyeshwa na wachezaji wangu.

"Kipindi cha kwanza tulianza taratibu, tofauti na tulivyofanya kipindi cha pili ambacho kilikuwa kizuri kwetu kwa kupata ushindi mkubwa tukiwa ugenini," alisema Moallin.


Moallin

Alisema ana matarajio makubwa ya timu yake hiyo katika kufikia malengo yao ya kuhakikisha wanashika nafasi tatu za juu na kuwa miongoni mwa timu zitakazowakilisha nchini michuano ya kimataifa.

Moallin alisema wanarejea nyumbani kujiandaa na mechi ijayo dhidi ya Trans Camp, mchezo wa hatua ya 32 bora ya Kombe la Shirikisho, utakaopigwa Uwanja wa Azam Complex, Chamazi nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam.

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATATU - 24/01/2022

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 15:15 | 5606 | Al Khaleej Club vs Al Jabalain | 2.14 | 3.09 | 3.24 |
| 15:50 | 5698 | Al Orubah vs AL Draih | 1.93 | 3.13 | 3.81 |
| 16:00 | 2099 | Crystal Palace U23 vs Liverpool U23 | 1.81 | 4.10 | 3.75 |
| 16:00 | 2740 | Wigan U23 vs Sheffield United U23 | 4.15 | 3.96 | 1.65 |
| 16:00 | 3055 | Rutsiro FC vs Gicumbi | 1.76 | 3.27 | 4.42 |
| 16:00 | 5772 | Police FC Rwanda vs Bugesera FC | 1.74 | 3.32 | 4.43 |
| 16:30 | 2077 | Birmingham U23 vs West Bromwich U23 | 3.87 | 4.16 | 1.66 |
| 18:00 | 3759 | Rivers United FC vs Heartland FC Owerri | 1.22 | 4.99 | 12.49 |
| 18:00 | 4584 | SP. Braga U23 vs Estoril Praia U23 | 2.18 | 3.32 | 2.93 |
| 18:30 | 1857 | Botosani vs Sepsi Osk | 2.55 | 2.99 | 2.84 |
| 18:30 | 2560 | Viseu vs Covilha | 2.14 | 3.27 | 3.22 |
| 18:45 | 5825 | Jeddah Club vs AL Nahdha | 1.95 | 3.14 | 3.72 |
| 19:00 | 5003 | West Ham U23 vs Leicester U23 | 1.40 | 4.83 | 5.60 |
| 19:00 | 5802 | Guinea vs Gambia | 2.17 | 2.93 | 3.72 |
| 20:00 | 2633 | AEK Larnaca vs Anorthosis Famagusta | 2.17 | 3.41 | 3.17 |
| 20:00 | 3047 | Hapoel Ramat Gan vs Hapoel Raanana | 2.49 | 3.04 | 2.94 |
| 20:00 | 4208 | Beitar Tel Aviv Ramla vs Hapoel Afula | 2.62 | 3.12 | 2.72 |
| 20:30 | 1273 | Asteras Tripolis vs Apollon Smyrnis | 1.52 | 3.89 | 6.30 |
| 21:00 | 2022 | Maracana CE vs Icasa CE | 1.56 | 3.62 | 5.41 |
| 21:00 | 3024 | Farul Constanta vs U Craiova SA | 1.56 | 3.69 | 5.90 |
| 21:30 | 1294 | Beitar Jerusalem vs Hapoel Tel Aviv | 3.27 | 3.17 | 2.09 |
| 21:30 | 1966 | Standard Liege U21 vs Anderlecht U21 | 3.66 | 3.85 | 1.76 |
| 21:30 | 1975 | AS Eupen U21 vs Westerlo U21 | 1.72 | 4.20 | 4.20 |
| 21:30 | 2353 | Crato EC CE vs Uniclinic CE | 3.40 | 3.55 | 2.06 |
| 21:30 | 3637 | Antwerp U21 vs KRC Genk U21 | 6.60 | 5.20 | 1.40 |
| 21:30 | 4610 | Cercle Brugge U21 vs KAA Gent U21 | 3.51 | 3.94 | 1.78 |
| 21:45 | 2704 | Din. Tirana vs KF Tirana | 4.22 | 2.97 | 1.90 |
| 22:00 | 1271 | Everton U23 vs Tottenham U23 | 3.94 | 4.14 | 1.65 |
| 22:00 | 1737 | Stoke City U23 vs Fulham U23 | 4.22 | 4.12 | 1.61 |
| 22:00 | 1988 | Aston Villa U23 vs Reading U23 | 1.27 | 5.78 | 7.13 |
| 22:00 | 2651 | Union Saint Gilloise U21 vs Lommel U21 | 1.60 | 4.06 | 4.35 |
| 22:00 | 3774 | Kmsk Deinze U21 vs Kortrijk U21 | 1.80 | 4.10 | 3.85 |
| 22:00 | 4155 | Mechelen U21 vs Club Nxt | 9.20 | 6.40 | 1.25 |
| 22:00 | 4271 | OH Leuven U21 vs Zulte Waregem U21 | 1.99 | 3.84 | 2.98 |
| 22:00 | 4347 | FC Oss vs Jong AZ Alkmaar | 2.12 | 3.47 | 3.08 |
| 22:00 | 4454 | Chelsea U23 vs Manchester City U23 | 3.51 | 3.94 | 1.78 |
| 22:00 | 4717 | Sunderland U23 vs Wolverhampton U23 | 2.88 | 3.55 | 2.12 |
| 22:00 | 4865 | Blackburn Rovers U23 vs Leeds United U23 | 2.27 | 3.85 | 2.50 |
| 22:00 | 5399 | Newcastle U23 vs Nottingham U23 | 2.13 | 3.85 | 3.05 |
| 22:00 | 5769 | Excelsior Virton U21 vs Beerschot Wilrijk U21 | 4.24 | 4.24 | 1.59 |
| 22:30 | 5704 | RWD Molenbeek U21 vs Oostende U21 | 3.46 | 4.03 | 1.78 |
| 22:45 | 1882 | Blackburn vs Middlesbrough | 2.60 | 3.09 | 2.70 |
| 22:45 | 2609 | Caen vs AC Ajaccio | 2.90 | 2.90 | 2.56 |
| 22:45 | 4503 | Annecy FC vs Concarneau | 2.29 | 3.04 | 3.13 |
| 23:00 | 2362 | Llaneros FC vs Orsomarso | 1.58 | 3.72 | 5.02 |
| 23:00 | 3084 | Catanzaro vs Palermo | 2.57 | 2.82 | 3.07 |
| 23:00 | 5316 | Almeria vs Eibar | 2.00 | 3.24 | 3.68 |
| 23:00 | 5762 | Real Sociedad B vs FC Cartagena | 2.54 | 3.18 | 2.69 |
| 23:15 | 3006 | Dunbeholden FC vs Montego Bay Utd | 1.96 | 3.19 | 3.62 |
| 23:15 | 5580 | Leixoes vs GD Chaves | 2.74 | 3.13 | 2.50 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo
Jumatatu Januari 24, 2022
Nipashe



## Ibrahimovic: Mbappe nenda tu Real Madrid

KASI...



Mshambuliaji wa Yanga, Fiston Mayele, akiambaa na mpira kabla ya kumsogezea Dickson Ambundo aliyeifungia timu yake bao pekee wakati wakishinda 1-0 dhidi ya Polisi Tanzania kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha jana. **PICHA: YANGA**

# YANGA SC YAPATIA GWARIDE LA POLISI

●●●Ambundo aichezesha 1-0 Arusha huku sasa ikiipiku Simba kwa pointi 10...

**Na Adam Fungamwango**

BAO pekee la dakika ya 63 lililofungwa na mchezaji mtokea benchi, Dickson Ambundo liliwawezesha vinara wa Ligi Kuu Tanzania Bara Yanga kuifunga Polisi Tanzania 1-0 jana kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha, ikiwa ni mechi ya tano mfululizo kupata ushindi na kuwa juu ya msimamo kwa pointi 35.

Ambundo ambaye ni bao lake la kwanza msimu huu kwa Yanga akisajiliwa kutoka Dodoma Jiji, aliachiwa mpira na Fiston Mayele ambaye alifanya kazi kubwa ya kumtoka beki Datius Peter kwa umbali mrefu upande wa kushoto mwa uwanja na kuingia ndani, kabla ya kumuachia mfungaji aliyekwamisha mpira kimyani kwa mguu wa kushoto.

Ni ushindi unaowaweka vinara hao juu kwa tofauti ya pointi 10 dhidi ya Mabingwa Watetezi, Simba wanaoshika nafasi ya pili kwa pointi 25.

Unakuwa ni wa tano mfululizo, ikiwa imefanya hivyo mara nne dhidi ya Prisons na Biashara United ikishinda mabao 2-1, ikiichapa Dodoma Jiji 4-0 na mara ya mwisho ikiichabanga Coastal 2-0 Jumapili iliyopita kwenye Uwanja wa Mkwakwani Tanga.

Vinara hao wamekuwa wakishinda mfululizo tangu walipotoka suluhu bila kufungana dhidi ya watani zao wa jadi, Simba Desemba 11, mwaka jana.

Mechi ilianza kwa Yanga kufanya mashambulizi yake kama kawaida kupitia pembeni, na hasa upande wa kulia ambako yupo Shaaban Djuma na Jesus Moloko wakiwa wanasubiriana mmoja akiwa na mpira na mwingine akimbie na kumegewa pande kwa mbele, staili ambayo msimu huu wanaitumia sana, lakini inavyoonekana Kocha Mkuu wa Polisi Tanzania, Malale Hamsini alikuwa ameifanyia kazi vizuri, akaweza kuidhibiti kwa kipindi chote cha kwanza akiwatumia wachezaji, Yahaya Mbegu, Tariq Simba na nahodha Mohamed Mmanga.

Kwa maana hiyo, Polisi Tanzania kazi yake ilikuwa ni kupambana na mfumo wa Yanga, kitu ambacho kilisababisha timu zote mbili kushindwa kufanya mashambulizi yoyote ya maana.

Shambulizi pekee hatari la Yanga dakika 45 za mwanzo lilitokea upande huo huo, wakati Moloko alipomtoroka Datius dakika ya 21, na kupiga krosi iliyounganishwa vema na Fiston Mayele akiwa katikati ya walinzi Juma Said 'Makapu' na Mmanga, lakini kwa bahati nzuri kwa wenyeji ukatoka nje kidogo ya lango.

Mastraika wa Polisi Tanzania kwa kipindi cha kwanza, mara chache walizofika walikuwa wakijigongagonga na kuishia kwenye miguu ya mabeki wa Yanga.

Kipindi cha pili baada ya kufanya mabadiliko ya kumtoa Farid Mussa na kumuingiza Ambundo, yaliifanya Yanga kubadilisha sehemu ya kupitisha mashambulizi na kupitia wingi ya kushoto badala ya kulia, Mayele akiamua kupitia pembeni na kusababisha bao hilo ambalo kwa kiasi kikubwa lilionekana kuwatoa mchezoni wachezaji wa Polisi Tanzania.

Mbali na Farid, Yanga ilimtoa pia Moloko na kumwingiza Chico Ushindi akicheza mechi yake ya kwanza ya Ligi Kuu Tanzania Bara baada ya kusajiliwa akitokea TP Mazembe akivaa jezi namba 25, iliyokuwa inavaliwa na Emmanuel Okwi alipoichezea timu hiyo kwa miezi sita msimu wa 2014/15.

Polisi Tanzania wanakuwa kwenye nafasi ya tano kwa pointi 18.

## Pablo apongeza wachezaji Simba

**Na Saada Akida**

LICHA ya kuambulia sare juzi dhidi ya Mtibwa Sugar, Kocha Mkuu wa Simba, Pablo Franco amesema wachezaji wake wamepambana na kutengeneza nafasi nyingi za kufunga, lakini bahati haikuwa kwao kupata ushindi katika mchezo huo wa Ligi Kuu Tanzania uliopigwa Uwanja wa Manungu, Turiani mkoani Morogoro.

Akizungumza na gazeti hili jana, Pablo alisema licha ya kutoka sare ya bila kufungana dhidi katika mchezo huo, ana kila sababu ya kuwapongeza wachezaji wake kwa namna walivyojituma.

Alisema ingawa uwanja haukuwa rafiki kwa wachezaji wake na aina ya soka linalochezwa na timu hiyo, lakini walipambana muda wote kutafuta ushindi.

"Ingawa tumecheza vizuri na wachezaji kupambana muda wote kuhakikisha tunapata ushindi, naamini haikuwa bahati kwetu kuondoka na pointi zote tatu," alisema Pablo.

Alisema walitengeneza nafasi nyingi kipindi cha pili ambazo wangeweza kuzitumia na kupata mabao kama nafasi ya dakika ya mwisho ya Shomari Kapombe.

"Pamoja na uwanja haukuwa rafiki kwa wachezaji na aina ya soka tunalocheza, lakini tulipambana muda wote kutafuta ushindi, nimependa jinsi walivyojituma, tumekuwa tukicheza mechi karibu karibu, wachezaji wanaumia hakuna jinsi tunapaswa kucheza na tunarudi Dar es Salaam, tutapata siku moja ya mazoezi kabla ya kwenda Kagera," alisema Pablo.

Simba itashuka tena dimbani Jumatano kuvaana na Kagera Sugar kwenye mechi yao ya kiporo itakayopigwa katika Uwanja wa Kaitaba mjini Bukoba.



9 770856 541002 >